Jumatatu Februari 3, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581941

epaper.ippmedia.com / www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com

**WALIOFAULU** usaili wa serikali waitwa kazini, waripoti ndani ya siku saba UKURASA 3



UKURASA 5

**SPIKA** wa Bunge ataka maombezi Uchaguzi Mkuu




UKURASA 7

**NEMC** yatoa tahadhari fukwe, miamba ya ziwa na mito mvua kubwa ijayo

JANGA SELIMUNDU

# Serikali yaja na mambo manne ya lazima, hiari

**WARAKA** waandaliwa, operesheni kuanza rasmi mwezi ujao; Kibatala, mawakili wenzake watoa neno... Endelea Ukurasa wa 2




## NHIF yatangaza vifurushi vipya

Na Mwandishi Wetu

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umetangaza vifurushi vipya vya bima katika makundi mawili ya Serengeti Afya na Ngorongoro Afya, kifurushi cha chini kikiwa ni Sh. 240,000 na cha juu Sh. 6,388,400 kwa mwaka.

NHIF imeainisha pia mafao yatakayotolewa kwa kila kifurushi na ukomo wa matumizi ya gharama za matibabu kwa mnufaika kwa mwaka ni Sh. milioni 22 kwa Kifurushi cha Serengeti Afya kwa anayelazwa na kutwa Sh. milioni tatu, huku Kifurushi cha Ngorongoro Afya ni Sh. milioni nane kwa anayelazwa na UKURASA 3

UKURASA WA 24

### RAMOVIC: KIKOSI YANGA SASA NI MOTO MKALI

BAADA ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Kagera Sugar, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amekisifu kikosi chake, akisema sasa kimekuwa moto wa kuotea mbali, akikiri...

### Wanajeshi wa Tanzania wauawa DRC, Rais wa Burundi atoa angalizo

UKURASA 19

MICHEZO SIMBA HII HATA 'NYUKI' INAUA TU UK. 24 KATUNI UK. 6

MAKALA MAALUM

JANGA SELIMUNDU

# Serikali yaja na mambo manne ya lazima na hiari

**Na Sanula Athanas**

SERIKALI imepokea mapendekezo yaliyotolewa na madaktari bingwa wa selimundu kukabili ugonjwa huo nchini, ikieleza kuwa baadhi hayatekelezeki kibajeti, pia katika uhusiano kijamii na utawala bora.

Desemba 31 mwaka jana, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu selimundu na madhara yake kimwili, kiuchumi na kijamii, takwimu za serikali zikionesha wanazaliwa watoto 14,000 wenye maradhi hayo nchini kila mwaka huku nusu yao wakipoteza maisha ndani ya miaka mitano ya kuzaliwa kwao.

Katika ripoti hiyo ya Nipashe, madaktari bingwa wa selimundu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam, Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando jijini Mwanza na Hospitali ya Rufani ya Benjamin Mkapa (BMH) jijini Dodoma walitoa mapendekezo matano kwa serikali.

Mapendekezo hayo ni pamoja na serikali kutunga sheria ya kuzuia kuoana kama hamjapimwa selimundu; wajawazito kupimwa selimundu wanapoanza kliniki; watoto kupimwa kama wana maradhi hayo mara tu wanapozaliwa; na kadi za kliniki za watoto kuwekwa alama ya kuwatambua wenye selimundu (SS) na waliobeba vinasaba vya maradhi hayo (AS).

Mabingwa hao pia walipendekeza serikali kutoa elimu kuhusu selimundu kwa jamii, ikiwezekana maradhi hayo yawe sehemu ya mtaala wa elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuoni nchini.

Mratibu wa Huduma za Selimundu, Himofilia na Magonjwa ya Damu - Wizara ya Afya, Dk. Asteria Mpoto na Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza - Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu wamezungumza na mwandishi wa habari hii kuhusu hoja za mabingwa hao wa selimundu.

Wote walikubaliana na mapendekezo hayo isipokuwa hoja ya kutunga sheria inayoweka sharti la kupimwa selimundu kabla ya kuoana na kujua hali ya vinasaba vya kinamama wote wanapoanza kliniki ya ujauzito.

**SHERIA YA SELIMUNDU**

Mkurugenzi Msaidizi Dk. Ubuguyu alisema pendekezo la kutunga sheria ya kuzuia wananchi kuoana kabla ya kupimwa selimundu halitekelezeki, akiwa na maelezo kuwa litaleta shida kijamii na utawala bora.

"Tukishatunga sheria hiyo, maana yake kuwe na adhabu. Tukishasema vijana wetu lazima wapimwe, waadhibiwe kwa kuoana bila kupimwa selimundu? Je, viongozi wa dini wataacha kweli kufungisha ndoa kisa wanaotaka kuoana hawajapimwa selimundu?

"Kumbuka asilimia 90 ya wanaoamua kufunga ndoa, walishaanza uhusiano zamani. Njia sahihi hapa ni kuelimisha vijana. Tuna kampeni ya 'Vunja Mduara wa Selimundu' iliyoanza mwaka jana, tunatoa elimu shuleni na vyuoni. Vijana wakishapata elimu na kupima, wanakuwa na uamuzi sahihi zaidi," Dk. Ubuguyu alisema.

Katika hilo, Mratibu wa Selimundu Dk. Asteria alisema hawajafikia hatua ya kutunga sheria kukabili selimundu na aliungana na Mkurugenzi Msaidizi Dk. Ubuguyu kwamba njia rahisi ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu maradhi hayo.

"Hata kwenye VVU (Virusi vya Ukimwi) hatujafikia hatua ya kuwa na sheria inayozuia anayeishi na VVU kuoana na mtu mwingine anayesihi na VVU. Kikubwa kinachotakiwa ni serikali tuendelee kuelimisha jamii yetu kuhusiana na huu ugonjwa. Wakishaelewa tu basi itakuwa rahisi kuukabili," Dk. Asteria alisema.

**WAJAWAZITO, WATOTO**

Kuhusu kuwapima selimundu wajawazito mara tu wanapoanza kliniki na baadaye watoto watakaowazaa, Dk. Ubuguyu alisema ni hoja yenye nia njema, lakini kibajeti haitekelezeki.

Mkurugenzi Msaidizi huyo alibainisha kuwa kwa wastani kila mwaka nchini kinamama milioni mbili hubeba ujauzito na kujifungua watoto milioni 2.4 (baadhi hujifungua pacha).

"Kipimo cha selimundu kinagharimu Sh. 11,000 kwa mtu mmoja. Sasa piga hesabu kwa idadi hiyo ya wajawazito na watoto wanaozaliwa, maana yake serikali itahitaji kuwa na zaidi ya Sh. bilioni 40 kwa mwaka kwa ajili ya kupima selimundu kwa wajawazito na watoto wachanga.

"Kulingana na bajeti yetu, hatutapima wajawazito na hatutapima watoto wote wanaozaliwa, bali katika kampeni yetu tutapima watoto wachanga kwenye maeneo yenye shida zaidi ya selimundu; mikoa ya Kanda ya Ziwa, Pwani na Kigoma.

"Tutaanza na mikoa ya Kanda ya Ziwa, na katika hili tuna ushirikiano na Serikali ya Marekani. Tutapima watoto 500,000 kwa mwaka. Upimaji watoto wachanga utaanza mwezi Machi mkoani Mwanza," Dk. Ubuguyu alisema.

Katika hilo, Mratibu wa Huduma za Selimundu Dk. Asteria alitaja mikoa yenye wagonjwa wengi, hata kuichagua kuanza nayo katika kampeni ya upimaji watoto wachanga, ni Mwanza, Kigoma, Geita, Shinyanga na Mara.

**KADI ZA KLINIKI**


Kuhusu kadi za kliniki za watoto kuwekwa alama ya kuwatambua wenye selimundu (SS), waliobeba vinasaba vya maradhi hayo (AS) na wasio na selimundu wala vinasaba vya maradhi hayo (AA), Dk. Asteria alisema hoja hiyo itafanyiwa kazi na wizara, akiwa na angalizo utekelezaji wake unagusa bajeti ya serikali.

"Zipo kadi za kliniki ambazo zilishatengenezwa na zinaendelea kutumika. Yatakapofanyika mapitio mengine ya kadi za kliniki katika miaka mitatu ijayo, watatushirikisha ili na sisi sasa tuweke vile vitu vya umuhimu ambavyo vinahitajika.

"Mpango upo wa kuhakikisha kwenye ile kadi tunaongeza huduma za sikoseli (selimundu) na ndiyo maana sasa hivi tunakwenda kupima watoto, ina maana tukishapima hawa watoto, nia yetu tuwapate kwenye kliniki," Dk. Asteria alisema.

**ELIMU SHULENI**

Kuhusu utoaji elimu ya selimundu katika jamii, Dk. Asteria alisema ndicho kipaumbele cha serikali, sasa wanaelekeza nguvu kwa wanafunzi wa shule za sekondari, vyuoni na kwa wanaohudhuria kliniki za selimundu hospitalini.




Selimundu inavyorithiwa kutoka kwa wazazi na namna ya kuiepuka.

"Vilevile, tuna waraka tunatarajia kuupeleka shule za sekondari na vyuoni kwa ajili ya kupima vijana mara tu wanapoingia shuleni na vyuoni. Vijana wanapoanza tu kidato cha kwanza na chuo wafanyiwe vipimo vya selimundu. Tupo kwenye huo mchakato.

"Si unajua, mtu anapokwenda kuanza kidato cha kwanza, kuna fomu ya daktari anapima haja ndogo, macho... sasa tunataka na sisi tuweke utaratibu apimwe vinasaba vya selimundu kwa sababu akitambua akiwa kidato cha kwanza, itamsaidia kuja kufanya uamuzi sahihi anapotaka kuoa au kuolewa.

"Wale ambao watakuwa wamebeba vinasaba vya selimundu (AS) wataendelea kupewa elimu ili watakapokuwa watu wazima, wasije wakaoa mtu mwingine aliyebeba vinasaba hivyo au mwenye selimundu tayari (SS)," Dk. Asteria alisema.

**MAWAKILI WALONGA**

Wakili wa Kujitegemea, Peter Kibatala anaungana na maofisa wa Wizara ya Afya kupinga pendekezo la kutunga sheria kuzuia kufunga ndoa kabla ya kupimwa selimundu.

Katika mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Wakili Kibatala alisema: "Wanachopaswa kufanya madaktari ni kutoa ushauri kwa jamii. Wawaeleze watu madhara yanayoweza kutokea wakizaa mtoto mwenye selimundu, zikiwamo gharama kubwa za matibabu ya ugonjwa huo.

"Magonjwa si selimundu tu, kuna magonjwa mengi; ugonjwa wa moyo na kisukari ni magonjwa ya kurithi. Je, nayo tuyatungie sheria? Zitatungwa sheria kwa magonjwa mangapi?"

Wakili Kibatala aliendelea kusema: "Ukitunga sheria, lazima uweke na utekelezaji wake. Hivyo, kabla ya kutunga sheria lazima ujue sheria hiyo ina mashiko kwa uhalisia au la.

"Wameshindwa kwenye VVU/Ukimwi, wataweza kwenye selimundu? Nia ni njema, lakini hauwezi kudhibiti maambukizi kwa kutunga sheria. Ni vyema serikali ikawekeza kwenye kufanya utafiti ili kupata ufumbuzi wa selimundu na magonjwa mengine. Tiba ya kutunga sheria ni kali sana, haitekelezeki!"

Wakati Kibatala akipinga ushauri huo wa madaktari, wakili mwenzake, Frank Chacha alisema mapendekezo ya mabingwa hao ni mazuri, akishauri muswada wa sheria ya kukabili selimundu uwasilishwe bungeni ili sheria itungwe.

"Hata kwenye CPA (Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai) na Sheria ya Ndoa kuna vifungu vinazuia ndugu kuoana, pia wenye magonjwa ya kurithi. Madaktari wako sahihi, itungwe sheria kuzuia wenye magonjwa ya kurithi kuoana, pia waliobeba vinasaba vya magonjwa hayo wasioane ili kupunguza maambukizi," alisema Wakili Chacha.

**KAULI ZA WANANCHI**

Godyfrey Kweka, mkazi wa mtaa wa Nyasaka "B", kata ya Kawekamo wilayani Ilemela, akizungumza na Nipashe kuhusu mapendekezo hayo ya madaktari, alisema hoja ya kutungwa sheria ya kupima selimundu kabla ya ndoa ina mashiko na italeta mafanikio katika kukabiliana na tatizo hilo.

"Familia inapopata mtu mwenye selimundu inapitia kipindi kigumu, wakati mwingine (ugonjwa huo) huchangia ndoa kuvunjika na malezi ya mtoto huyo kubaki kwa mzazi mmoja.

"Kama unaweza kukimbia familia kisa mtoto amezaliwa na tatizo, kwa nini usipime kabla ya kuingia katika uhusiano ili kuepuka kupata mtoto wa hivyo ambaye ataishi kwa maumivu katika maisha yake yote?" Kweka alihoji.

Sundi Charles, mkazi wa Isamilo, wilayani Nyamagana, aliunga mkono pendekezo la mabingwa wa selimundu la kutunga sheria, akiamini hatua hiyo itapunguza au kumaliza tatizo la maradhi hayo nchini.

"Japokuwa italeta shida kwenye uhusiano wa watu kuvunjika, mimi ninaona ni heri uhusiano au uchumba uvunjike kuliko kuingia katika ndoa kisha mkapata watoto wenye selimundu mkazidi kuongeza tatizo ambalo linagharimu fedha nyingi katika matibabu yake. Mtoto mwenye selimundu anapitia mateso makubwa," Charles alishauri.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, gharama za kupandikiza uloto nchini, ambayo ndiyo tiba ya selimundu, zinaanzia Sh. milioni 50 hadi 55. Kwa sasa nchini matibabu hayo yanatolewa BMH pekee. Mgonjwa asipopandikizwa uloto, fedha hizo zinatosha gharama za kliniki ya ugonjwa huo kwa miaka mitano tu kwa kila mgonjwa.

**SELIMUNDU NI NINI?**

Selimundu, kama ilivyotolewa ufafanuzi na Bingwa wa Maradhi ya Watoto katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Evance Godfrey, ni ugonjwa wa kuzaliwa nao kutokana na kurithi kutoka kwa wazazi kupitia vinasaba.

Ni tatizo la muda mrefu kwenye seli nyekundu za damu ambalo husababisha baadhi ya seli nyekundu za damu kuwa na umbo lisilo la kawaida. Badala ya kuwa na umbo linalofanana na diski, zinakuwa na umbo kama la nusu mwezi (mwezi mwandamo) ambalo husababisha seli nyekundu za damu kuvunjika kwa urahisi na zisitoshee vizuri katika mishipa midogo ya damu ili kusafirisha oksijeni.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@*

## HABARI KITAIFA

# NHIF yatangaza vifurushi vipya bima ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umetangaza vifurushi vipya vya bima katika makundi mawili ya Serengeti Afya na Ngorongoro Afya, kifurushi cha chini kikiwa ni Sh. 240,000 na cha juu Sh. 6,388,400 kwa mwaka.

NHIF imeainisha pia mafao yatakayotolewa kwa kila kifurushi na ukomo wa matumizi ya gharama za matibabu kwa mnufaika kwa mwaka ni Sh. milioni 22 kwa Kifurushi cha Serengeti Afya kwa anayelazwa na kutwa Sh. milioni tatu, huku Kifurushi cha Ngorongoro Afya ni Sh. milioni nane kwa anayelazwa na Sh. milioni mbili kwa asiyelazwa.

Kwa mujibu wa tangazo lililowekwa kwenye tovuti ya NHIF, watoto wa miaka 0-17, mmoja analipa Sh. 240,000 kwa Kifurushi cha Ngorongoro Afya na Sh. 660,000 kwa Kifurushi cha Serengeti Afya.

Umri wa miaka 18-35 mgawanyo ni kwa mtu mmoja; wanandoa; mtu mmoja na mtoto mmoja; mtu mmoja na watoto wawili; mtu mmoja na watoto watatu; mtu mmoja na watoto wanne; wanandoa na mtoto mmoja; wanandoa na watoto wawili; wanandoa na watoto watatu; na wanandoa na watoto wanne.

Gharama kwa kila kundi kwa Kifurushi cha Ngorongoro Afya zinaanzia Sh. 432,000 hadi 1,684,800 huku Serengeti Afya zikiwa ni kuanzia Sh. 792,000 hadi 3,880,800.

Gharama kwa kundi la miaka 36-59 kwa Kifurushi cha Ngorongoro Afya zinaanzia Sh. 540,000 hadi Sh. 1,890,000 huku kwa Kifurushi cha Serengeti Afya zinaanzia Sh. 1,620,000 hadi Sh. 5,454,000.

Gharama kwa umri wa miaka 60 kuendelea kwa Kifurushi cha Ngorongoro Afya ni Sh. 708,000 kwa wanandoa, huku wanandoa na mtoto mmoja ni Sh. 1,345,200. Kifurushi cha Serengeti Afya kwa umri huo kwa wanandoa ni Sh. 3,336,000 na wanandoa na mtoto mmoja ni Sh. 6,336,400.

Mafao yanayotolewa kwa wanachama wa vifurushi vya bima ya afya ikiwa na mafao tofauti kwenye mabano (idadi ya huduma) ambayo ni Kifurushi cha Serengeti Afya; huduma za dawa (907), upasuaji mkubwa na mdogo (565), vipimo vya maabara na uchunguzi (315), vifaa tiba visaidizi (17), ada ya kujiandikisha na kumwona daktari (inapatikana) na huduma za kulazwa (inapatikana).

Kwa Kifurushi cha Ngorongoro Afya; mafao ni kila eneo kwenye mabano ni huduma za dawa (286), upasuaji mkubwa na mdogo (60), vipimo vya maabara na uchunguzi (88), vifaa tiba visaidizi (hakuna), ada ya kujiandikisha na kumwona daktari (inapatikana); na huduma za kulazwa (inapatikana).

Katika tovuti hiyo imeandikwa: "Vifurushi vya Bima ya Afya vya NHIF ni mpango unaowezesha mwananchi mmoja mmoja au familia kuchagua na kuchangia huduma za matibabu kabla ya kuugua na kisha kuwa na uhakika wa matibabu kwa kutumia bima ya afya bila kikwazo."

**Gharama kwa kundi la miaka 36-59 kwa Kifurushi cha Ngorongoro Afya zinaanzia Sh. 540,000 hadi Sh. 1,890,000 huku kwa Kifurushi cha Serengeti Afya zinaanzia Sh. 1,620,000 hadi Sh. 5,454,000.**

Ppia kumeainishwa faida za kujiunga na vifurushi vya bima ya afya kwamba ni wigo mpana wa huduma za matibabu za msingi, kubingwa na bingwa bobezi; punguzo la asilimia 10 ya mchango wa mtegemezi kwa wanaojiunga kwa familia.

Faida nyingine ni matibabu nchi nzima katika vituo vya matibabu zaidi ya 10,000 kuanzia ngazi ya zahanati hadi Hospitali ya Taifa, na kwamba utaratibu wa rufani utatumika katika Hospitali za Rufani za Kanda na Taifa.

Taarifa hiyo inataja mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya kujiunga na vifurushi vya bima ya afya na kwamba kila mnufaika atakuwa na ukomo wa matumizi ya gharama za huduma kwa mwaka, hivyo wanachama wanashauriwa kufuatilia matumizi yao kwa ukaribu na kuepuka matumizi holela.

Mwanachama atasubiri kwa siku 30 kabla ya kuanza kupata huduma baada ya kukamilisha taratibu za usajili na kulipia; mwanachama atatakiwa kuhuisha uanachama wake ndani ya siku 30 baada ya kufika ukomo wa uanachama wake.

Pia mwanachama atakayeshindwa kuhuisha uanachama wake ndani ya kipindi husika atahesabiwa kama mwanachama mpya na atakuwa na muda wa kusubiria kwa siku 30.

**TOTO AFYA**

Taarifa kwenye tovuti hiyo inaeleza mafao ya wanufaika wa Toto Afya kwa makundi yanayolipa Sh. 50,400 kuwa ni huduma ya kumwona daktari wa kawaida, bingwa na bingwa mbobezi; huduma za vipimo vya maabara, CT-Scan, MRI, Ultra Sound, X-ray, ECHO na ECO; baadhi ya dawa za magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama kisukari, shinikizo la damu, selimundu, magonjwa ya moyo na magonjwa ya figo.

Nyingine ni huduma za kulazwa wodi ya kawaida, chumba cha wagonjwa mahututi (ICU na HDU); baadhi ya huduma za upasuaji mkubwa na mdogo wa magonjwa ya tumbo; huduma za kuchuja damu; huduma za saratani; huduma ya kinywa na meno kama kuziba, kung'oa, kusafisha na meno bandia; huduma za mazoezi tiba na mtengamao; huduma za dharura na vifaa tiba pandikizi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@***

# Walimu waliofaulu usaili serikalini waitwa kazini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Rais - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imewaita waombaji waliofaulu usaili wa nafasi za kazi mbalimbali kuchukua barua zao za kupangiwa vituo vyao ndani ya siku saba baada ya tangazo hilo.

Tangazo hilo lililotolewa juzi na Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, likieleza kuwa Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma anawaarifu waombaji kazi wa nafasi mbalimbali waliofanya usaili kati ya tarehe 24-02-2024 na tarehe 17-01-2025 kuwa matokeo ya waombaji kazi waliofaulu usaili huo ni kama yalivyoorodheshwa katika tangazo hilo.

Orodha ya majina hayo pia inajumuisha baadhi ya wasailiwa waliokuwa kwenye kanzidata kwa kada mbalimbali ambao wamepangiwa vituo vya kazi baada ya nafasi kupatikana. Waombaji waliofaulu usaili wanatakiwa kuchukua barua za kupangiwa kituo cha kazi katika Ofisi za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma zilizoko Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Vilevile, waombaji kazi waliofaulu usaili na kupangiwa kituo cha kazi wanatakiwa kuripoti kwa mwajiri katika muda ambao umeainishwa kwenye barua za kupangiwa kituo cha kazi wakiwa na vyeti halisi vya masomo kuanzia kidato cha nne na kuendelea ili vihakikiwe na mwajiri kabla ya kupewa barua ya ajira.

Mbali na hilo, kwa wale ambao majina yao hayako katika tangazo hilo, watambue kuwa hawakupata nafasi/hawakufaulu usaili, hivyo wasisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.


**KIBAIGWA AUCTION MART**
**P.O.BOX 20, DODOMA**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KIBAIGWA AUCTION MART**

KWA IDHINI NILIYOPEWA NA KAMPUNI YA IMARISHA MAISHA FINANCIAL SERVICES LTD. TUTAUZA GARI MOJA AINA YA VOLKSWAGEN TIGUAN YENYE NAMBA ZA USAJILI T 510 EDT MALI YA FRANK MORAN MWAHALENDE , BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 14/02/2025 MAENEO YA NYERERE SQUARE SAA 10:00 ASUBUHI

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NO. 0688 729841**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MTWARA, LINDI NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA MADABA, NAMTUMBO NA TUNDURU.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma katika Halmashauri za Wilaya za Madaba, Namtumbo na Tunduru tarehe 28 Januari hadi 03 Februari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumanne tarehe 28 Januari hadi siku Jumatatu tarehe 03 Februari, 2025
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa leo tarehe 20 Januari, 2024 na:**

**Christina P. Ballali**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

# TAKUKURU yaibua 'madudu' kwenye miradi ya bilioni 28/-

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Tabora, Abnery Mganga amesema katika uchunguzi waliofanya mkoani mwake, wamebaini dosari katika miradi ya maendeleo minane kati ya 11 yenye thamani ya Sh. bilioni 28.

Mganga alibainisha hayo juzi wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari na kueleza kuwa miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa shule (vyumba vya madarasa) katika shule za msingi na sekondari kupitia mradi wa SEQUIP na BOOST iliyotekelezwa katika wilaya zote mkoani Tabora.

Mganga alisema kuwa baadhi ya mafundi waliobainika kutokuwa na uwezo, tayari wametoa maelekezo kusitishwa mikataba yao pamoja na wale walioshindwa kutekeleza kazi zao ndani ya wakati na kutafutwa wengine wenye uwezo wa kutekeleza kazi hizo.

"Tumebaini dosari nyingi katika miradi hii ikiwamo kutumika vifaa visivyo na ubora ambapo tumeagiza kusitishwa mara moja kwa kazi iliyokuwa inafanyika na kuelekeza wahusika wakafanye uthibitisho wa vifaa hivyo," alisema.

Alizitaka ofisi za halmashauri ambazo miradi yao imetekelezwa katika maeneo yasiyo na huduma za kijamii, kuongeza fedha za kupeleka huduma hizo ili kutokuathiri gharama zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji miradi hiyo pamoja na waandaaji kuandaa bajeti inayoakisi uhalisia wa mahitaji ya eneo husika.

# 'Wazazi wasiowajibika kwa watoto washtakiwe'

**Na Elizabeth Zaya**

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Muhange wilayani Kakonko, mkoa wa Kigoma wamewashauri wanasheria walio katika Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, kuwabana wazazi wanaoshindwa kutoa huduma za malezi kwa watoto na hivyo baadhi yao kukatisha masomo yao.

Walisema wapo watoto wengi ambao wanashindwa kwenda shuleni au kukatisha masomo yao kutokana na wazazi wao kushindwa kutoa matunzo na mahitaji yao ya msingi.

Ni rai waliyotoa juzi mbele ya mawakili na wanasheria kwenye kampeni ya kutoa msaada kisheria iliyofanyika kwa siku 10 wilayani Kakonko, mmoja wa wanafunzi hao anayesoma kidato cha nne katika shule hiyo ya Muhange, Joseph Edward, akisema baadhi ya wazazi hawatoi mahitaji muhimu ya watoto wao zikiwamo sare za shule, madaftari na hawalipii michango midogo ya shule na hivyo kusababisha wanafunzi wengine kukata tamaa na kuacha kwenda shuleni.

Adela Charles, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule hiyo, alisema: "Unakuta mwanafunzi anaweka nia na dhamira ya kusoma kwa bidii ili afanye vizuri, apate alama ambazo zitamwezesha kujiunga na masomo ya elimu ya juu lakini kutokana na yale anayopitia, anakosa sare, madaftari na mahitaji mengine, mpaka anapatwa na msongo wa mawazo, anashindwa kufanya vizuri kwenye masomo na mwisho wa siku anapata matokeo mabaya.

"Si hivyo tu, wengine huwa wanaona aibu, kwa mfano anakwenda shuleni nguo zake zimechakaa au zimechanika, anaamua kuacha kwenda kabisa. Kwa hiyo tunaomba kama kuna sheria inayowabana wazazi wazembe wa namna hii, wawe wanachukuliwa hatua za kisheria ili wasiwakwamishe watoto wao kutimiza ndoto zao kielimu," alisema.

Akitoa mada ya ukatili kwenye kampeni hiyo, Ofisa Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi Wilaya ya Kakonko, Getrude Silvestre alisema kitendo cha wazazi kushindwa kugharamia mahitaji ya wanafunzi hao kinasababisha watoto kupatwa na msongo wa mawazo.

Ni ukatili wa kisaikolojia ambao unaweza kuchangia watoto hao kufanya vibaya kwenye masomo yao.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko, Meshack Kamonongo alisema lazima jamii ichukie ukatili wowote kwa watoto ikiwamo vitendo vya ubakaji na ulawiti, mimba kwa wanafunzi sambamba na wazazi kutelekeza familia, akiwataka wanafunzi hao kutoa taarifa kwa vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa au kuviona.




Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kimataifa Academic, wakifanya matembezi ya kuhamasisha kuchangia fedha kwa ajili ya kusaidia matibabu ya watoto wenye saratani, Upanga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Shule yawachangia mil 14/- watoto wanaougua saratani

**Na Jenifer Gilla**

SHULE ya Sekondari ya Academic International imetoa msaada wa Sh. milioni 14 kwa ajili ya kusaidia matibabu ya watoto wanaougua saratani nchini.

Mkuu wa Shule hiyo, Shyama Santhosh, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa matembezi ya kuhamasisha uchangiaji fedha kwa ajili ya kuwasaidia watoto wanaougua saratani, ikiwa ni sehemu ya Kampeni ya Piggy Bank inayoendeshwa na Taasisi ya Tumaini la Maisha.

Matembezi hayo ambayo yalianzia viwanja vya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi (JWTZ) Upanga hadi Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), yameratibiwa na shule hiyo kwa kushirikiana na Benki ya CRDB, JWTZ na Taasisi ya Tumaini la Maisha.

Mkuu wa Shule hiyo, Shyama Santhosh, ameitaka jamii kuwa na moyo wa kujitolea kusaidia watoto wenye uhitaji kutoka kwenye makundi mbalimbali, ikiwamo wagonjwa ili kurahisisha upatikanaji wa huduma na kuwarudishia tumaini.

Alisema lengo la matembezi hayo ni kuhamasisha jamii kuchangia watoto wanaougua saratani. Mbali na kuratibu matembezi hayo, shule hiyo ilichangia Sh. 14,080,000 kwa Taasisi ya Tumaini la Maisha kwa ajili ya mahitaji ya watoto hao, zikiwamo gharama za matibabu.

"Hii ni mara ya pili tunashiriki katika kampeni hii na safari hii tumeshirikisha wanafunzi katika matembezi, ili kuwajengea moyo wa kutoa na kuisaidia jamii, lengo ni kutengeneza kizazi chenye upendo na kujitolea, kusaidia makundi mbalimbali yenye mahitaji," alisema.

Eliwangu Mlaki kutoka Taasisi ya Tumaini la Maisha, aliishukuru shule hiyo kwa fedha walizowapa kwa kuwa zitakwenda kusaidia matibabu ya watoto wanaougua ugonjwa huo wanaopata matibabu MNH na hospitali nyingine 13 nchi nzima.

Pia aliwashukuru wadau wengine wanaowaunga mkono katika kampeni hiyo na kuratibu matembezi yanayolenga kuhamasisha jamii kutoa kuchangia fedha kwa kundi hilo.

Meneja Uhusiano wa Benki ya CRDB, Lulu Meru, alisema wameunga mkono matembezi hayo kwa ajili ya kukusanya fedha za kuwasaidia watoto wenye saratani ili ziwasaidie katika mahitaji yao na kuwapa tabasamu.

Alisema kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wanasaidia jamii kupitia sekta mbalimbali ikiwamo afya, hivyo wameguswa kuona kuwa katika nchi kuna watoto wanaugua ugonjwa huo.

"Sisi kama CRDB, benki ya wazalendo, tunafanya kazi karibu na jamii, tumeona tushiriki matembezi haya, ili kuhamasisha jamii kuchangia kiasi hicho cha fedha," alisema.

Mwenyekiti wa Shule hiyo, Balozi Alli Siwa, aliwapongeza wanafunzi na wazazi walioguswa na kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia watoto wanaougua saratani na kuwa ni matumaini yake mkakati huo utakuwa mfano wa kuigwa na jamii.

Meja Jenerali Wilbert Ibuge alisema japokuwa matembezi hayo ni mafupi, yana maana kubwa kwa kuwa lengo lake ni kutoa tabasamu na matumaini kwa watoto wanaougua saratani ambao wengine hawana uwezo wa kupata mahitaji muhimu.

## HABARI KITAIFA



Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson akishiriki ibada ya jumapili katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Kimara, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati yaundwa uchunguzi wageni wanaofanya umachinga Kariakoo

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo ameunda kamati maalumu ya watu 15 kuchunguza wimbi la wageni wanaofanya biashara za uchuuzi 'machinga' katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam.

Ni hatua iliyochukuliwa siku chache baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kusikia kilio cha Watanzania hususan wafanyabiashara wa Kariakoo, kuhusu kero hiyo.

Dk. Jafo amesema kamati hiyo itakayokuwa chini ya Mwenyekiti wake, Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga, itafanya kazi hiyo ndani ya mwezi mmoja na kuwasilisha taarifa yake.

Alitangaza hayo jijini Dar es Salaam jana alipokutana na wafanyabiashara wa Kariakoo, akiwamo Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Hamis Livembe, Mwenyekiti wa Soko la Kariakoo na Halmashauri Kuu ya uongozi wa soko hilo.

"Hivi karibuni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokea kilio cha wananchi wa Kariakoo, Dar es Salaam na watanzania hususan wafanyabiashara, suala la hivi sasa kuwapo mwingiliano wa wageni wengi ambao huwa wanakuja na ajenda ya uwekezaji, kwa bahati mbaya uwekezaji wao hauakisi suala zima la uwekezaji.

"Wanapofika nchini changamoto iliyojitokeza ni kwamba, wanashiriki katika shughuli nyingine ambazo zipo nje ya utaratibu wa uwekezaji. Baadhi ya shughuli hizo ni kufanya biashara za rejareja za kimachinga, mwisho wa siku huathiri mwenendo wa biashara kwa watanzania," alisema.

Waziri huyo alisema hiyo imekuwa kero kubwa kwa wafanyabiashara na kuathiri biashara zao, ikizingatiwa Tanzania inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni ambapo mgeni yeyote au mtu anapaswa kufanya biashara kulingana na maelekezo ya serikali.

"Kuna wimbi la wageni ambao wanafanya biashara tofauti na utaratibu wa kisheria, hivyo huleta kero kwa wafanyabiashara wazawa na kuathiri mitaji yao na kuwa na vijana waliofilisika kutokana na wengine wameanzisha magodauni na kuleta biashara na kuuza rejareja," alisema.

Alisisitiza kuwa jambo hilo halivumiliki, hivyo anatekeleza maelekezo ya Rais Samia akiwa waziri mwenye dhamana kwa kuunda kamati maalumu ya watu 15 kuondoa changamoto hiyo inayowakabili wafanyabiashara.

Dk. Jafo alisema Mwenyekiti wa kamati hiyo, Profesa Edda anaamini atasaidia kwa kuwa amebobea kwenye masuala ya biashara, akisaidiwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa wizara hiyo, Sempeho Manongi (Katibu wa Kamati).

Wajumbe ni Naibu Kamishna wa Polisi, Francis Maro, Naibu Kamishna Uhamiaji, Kigongo Shile, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Latifa Khamis.

Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gilead Teri, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Godfrey Nyaisa, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani (FCC), William Erio, Teddy Frank, Zubeda Masoud, Ofisa Kazi Mwandamizi wa Dar es Salaam, Eliuluma Mabelia, Raphael Maganga kutoka sekta binafsi, Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Kariakoo, Severine Mushi na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Hamis Livembe.

Alitaja hadidu za rejea zinazojumuisha utafiti wa kina Soko la Kariakoo likiwa kama la mfano, kubaini ukubwa wa tatizo la wageni kufanya biashara nchini ambalo linaathiri ajira kwa watanzania.

Pia watakagua vibali vya wageni na uhalali wake, kuchunguza wageni kupewa vibali na leseni za biashara zinazofanywa na watanzania.

Dk. Jafo alisema kamati hiyo itaangalia masuala ya dharura ni nini kifanyike kwa haraka kutatua tatizo hilo kwa kuainisha njia za haraka na muda mfupi, chanzo cha tatizo na namna ya kuepuka.

Aliwaomba wafanyabiashara kuwa watulivu wakati kamati hiyo inafanya kazi yake ambayo itasaidia si tu sekta ya biashara, bali pia na sekta nyingine kuweka misingi ya utekelezaji.

Mwenyekiti wa Soko la Kariakoo, Livembe alisema kutokana na maelekezo ya Rais Samia, changamoto ya kuwapo wageni wanaofanya biashara za uchuuzi itapatiwa ufumbuzi.

Livembe alipongeza serikali kwa hatua iliyochukua ndani ya muda mfupi baada ya kutolewa kwa maelekezo na kuundwa kamati hiyo ambayo imepewa siku 30 kuwasilisha mapendekezo ya nini kifanyike.

# Tulia ataka maombezi Uchaguzi Mkuu 2025

**Na Elizabeth Zaya**

SPIKA wa Bunge, Dk.Tulia Ackson amewaomba watanzania kuombea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, ili wapatikane viongozi bora na wema watakaoongoza taifa liendelee kuwa na amani.

Dk. Tulia alitoa rai hiyo jana alipokaribishwa kusalimia waumini katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Kimara mkoani Dar es Salaam wakati wa ibada ya Jumapili.

Alisema anaamini watanzania wamekuwa wakimwombea Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wote, lakini kwa mwaka huu ni vyema wakaelekeza maombi yao kwenye uchaguzi huo.

"Nidhahiri kwamba mnaliombea taifa hili na mnamwombea Rais Samia Suluhu Hassan, sasa wakati mwingine huwa mnamsikia akiwashukuru viongozi wa dini kwa ujumla wao kwamba wanaliombea taifa hili na anaomba waendelee kuliombea na kumwombea, lakini na ninyi wana-Kimara ni sehemu ya ambao wanamwombea mema Rais.

"Na niwaombe kipekee, tuongeze maombi zaidi kwa sababu yeye ndiye nembo ya taifa letu, ndiye Rais wetu, ndiye kiongozi wetu na pamoja na mambo mengine, mimi ni mwumini wa hapa sawa, lakini mwaka huu ni wa uchaguzi. Kwa hiyo ni vizuri watu wa Mungu tukatulia mbele za Mungu na kwa kweli kufanya yaliyo bora kabisa, siwezi kutumia madhabahu kusema mambo ya siasa na huwa sipendi kufanya hivyo.

"Lakini ni muhimu wewe umchaye Bwana, kwa sababu Biblia inasema 'maombi ya mwenye haki yafaa sana, tena ukiomba kwa bidi'. Sasa wewe mwana-Kimara maombi yako yafaa sana, tena ukiomba kwa bidi. Liombee taifa hili liendelee kuongozwa vizuri, viongozi wawe bora, ili na wewe maisha yako yastawi katika taifa hili," alisema Dk. Tulia.

Aliwataka wananchi kuacha kujiweka pembeni na kuendelea kubisha kwa kila jambo linalofanyika, akiwa na ufafanuzi: "Usijiweke tu pembeni ukafikiri wewe utakuwa tu kila wakati ubishe kila jambo linalofanyika, ubishe kila siku, kila jambo. Wewe unayemcha Mungu, kazi yako ni kupiga magoti, kwa sababu viongozi watakaochaguliwa Biblia imekuagiza kuwaheshimu wenye mamlaka.

"Na ili umheshimu, basi mwombe Mungu atupe viongozi bora, wema, watakaolifanya taifa letu liendelee kuwa na amani, na mimi ninaamini tutaendelea kufanya vyema kwa kadri Mungu atakavyotujalia. Kwa hiyo pamoja na shukrani zote hizi kwamba mnamwombea Rais, mnaniombea mimi na viongozi wote, mnaombea amani taifa hili, lakini mwaka huu tuombee uchaguzi, Mungu atupe viongozi bora, viongozi wema."

Oktoba mwaka huu Tanzania inatarajiwa kufanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Tayari Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) inafanya maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapigakura.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customer-relations@***


(RULE 5)

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MPANDA AT MPANDA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 2169 OF 2025 In the Matter of the Estate of the Late FARAJA DICKSON NYAMWANJI

And

In the Matter of Application for ADMINISTRATION By DICKSON MATONYA NYAMWANJI

FORM 58
GENERAL CITATION
(RULE 75)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 30TH day of JANUARY, 2025

Dated at Dodoma this 14 TH day of FEBRUARY 2025

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
MPANDA - KATAVI

KUPOTEA KWA CHETI



**JUDITH NUNGU MKIKA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha Chuo chenye namba za usajili **sgd/bba/19/68670** kilichotolewa na chuo cha Tia Mwaka 2022. Yeyote atakaekiona atoe taarifa Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/ILA/13115/2025**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya CHAMWINO MJINI

Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA

Shauri a madai Na 291/2024

Jina la Mdai: MUSA KAPO

Jina la Mdaiwa: ALLY SOGORA

KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuniya 18
yakanunizataratibuMadaikatikamahakamazaMwanzo)

Kwa:ALLY SOGORA

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba Unaamriwa na Jamhuri uhudhurie Mahakamani hapa ili ujibu madai ya fedha 6,400,000/-

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 03 Mwezi 02 Mwaka 2025 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. ANGALIZO:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 28 Mwezi 01 Mwaka 2025

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO-MJINI
DODOMA

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Umakini kwa waamuzi unahitajika mzunguko wa pili Ligi Kuu Bara

**MZUNGUKO** wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara umeanza, huku kila timu ikijidhatiti kupata matokeo mazuri ili kufikia malengo iliyojiwekea.

Kuna timu zitauhitaji ushindi kwa udi na uvumba, zipo zinazotaka kumaliza ndani tu timu nne za juu ili kupata angalau nafasi ya kucheza mechi za kimataifa mwakani na zile ambazo zitakuwa zinakusanya pointi kwa ajili ya kutaka kubaki Ligi Kuu.

Hata hivyo, ni lazima mwishoni zipatikane timu mbili zitakazoshuka daraja na mbili zitakazocheza mechi za mchujo. Lakini ni baada ya kufanya vibaya kwenye michezo ya Ligi Kuu hatua iliyobaki.

Tunataka timu zitakazoshuka na kwenda 'play off', ziwe kweli zimeshuka kutokana na uwezo wao mdogo na si kukandamizwa kwa sababu zozote zile.

Zitakazokwenda kucheza michuano ya kimataifa ziwe zilizofuzu kweli kweli na si kupelekwa kwa kusaidia, matokeo yake kwani timu nyingi zinatolewa mapema na kubaki chache, kitu ambacho si afya kwenye soka la Tanzania.

Hata bingwa, anatakiwa awe ni yule ambaye kweli ameupata kwa kuutolea jasho na si kubebwa na waamuzi ambao wakati mwingine wamekuwa wakilaumiwa kwa kuchezesha kinyume cha kanuni za soka duniani ama kwa upendeleo, woga, maagizo ama hata rushwa ambayo mara nyingi imekuwa vigumu kuthibitishwa, kitu ambacho kinazalisha kile kinachoitwa makosa ya kibinadamu.

Kwa maoni yetu, tunawataka waamuzi wote watakaochezesha mechi za mzunguko wa pili wachezeshe kwa makini na haki, bila kuipendelea au kuionea timu yoyote.

Klabu hizi tunaziona zimekuwa zikihangaika kupata makocha wazuri kwa kuwalipa pesa nyingi, kufanya usajili mzuri, lakini wakati mwingine wanaangushwa na kosa moja la mwamuzi ambalo wakati mwingine linasababisha si timu kupoteza mechi, bali hata makocha kutimuliwa.

Hiki ni kipindi hatari cha makocha ambao wataokena hawafikii malengo ya timu kutimuliwa, sasa waamuzi wasiwe ndio chanzo cha kuwakosesha wenzao mkate kwa manufaa yao, uzembe, au kutokuwa makini.

Tunaona itabidi waachwe makocha watimuliwe kutokana na kushindwa wao wenyewe, si kwa mtu mwingine kumfanya aonekane hawezi, hii kwetu ni dhambi kubwa na haivumiliki.

Kwa waamuzi wenyewe angalau husimamishwa na baadaye kurudishwa uwanjani, lakini makocha wakishatimuliwa hawawezi kurudishwa tena kwenye klabu ile, badala yake atakaa ili kuona ni sehemu gani anahitajika, wakati mwingine hili huchukua muda mrefu, huku akiwa hana kazi yoyote.

Viongozi wa klabu hata zile zinazoitwa au kujiinda ndogo, mzunguko huu wa pili zimeonekana kujitutumua kusajili wachezaji wazuri na baadhi ya makocha bora kutoka ndani na nje ya nchi, tunadhani sasa ni wakati wa kuuacha mpira wenyewe uchezeke kiwanja na uamue nani mshindi kwa uwezo na si vinginevyo.


Kinyume cha hayo ni kutozitendea haki klabu na viongozi wao, ambao huingia gharama kubwa ya kuwalipia vibali vya kazi na ukaazi wachezaji wa nje kwa ajili ya kuzipigania timu zao, halafu mwamuzi anakuja kuingia na matokeo yake mfukoni.

Tunawashauri waamuzi waingie uwanjani kama mahakimu wa haki na haki ionekane ikitendeka kweli, kwani kwa tunavyojua mzunguko wa pili utakuwa mgumu mno na ushindani mkubwa, pointi moja tu iliyopatikana au kukosekana kwa makosa ya refa, inaweza kuipatia timu ubingwa isiyostahili, au kuinyima iliyotakiwa iupate.

Lakini inaweza kuishusha timu daraja ambayo ilitakiwa kubaki, kuibakisha iliyostahiki kwenda Ligi ya Championship, vile vile kuzipa timu dhaifu nafasi za kucheza Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho na kuziacha ambazo zingekwenda kuliwakilisha vema taifa.

Bingwa bora, wawakilishi wa nchi, zikazoshuka daraja na kubaki, wote wako kwenye mikono ya waamuzi watakaoamua kuchezesha kwa kufuata sheria zote 17 soka ulimwenguni. Hivyo tunazitakia timu zote kila laheri kwenye mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara huku tukitaka 'Mchezo wa Haki (Fair Play), kama kaulimbiu ya Fifa inavyosema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# KenGold itaweza kumdhibiti 'chautundu' Morrison atulie?

Na Adam Fungamwango

**KUTAMBULISHWA** kwa Bernard Morrison KenGold FC, hilo ni jambo moja, je inaweza kumdhibiti 'chautundu' huyo?

Hili ndilo jambo linaloulizwa na kusubiriwa na mashabiki wengi wa soka nchini. Ni baada ya winga huyo raia wa Ghana, kujiunga na timu hiyo kwa wachezaji waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Kinachowafanya mashabiki wengi waulizane na kufikiria hivyo ni tabia ya utundu aliyonayo mchezaji huyo licha ya kuwa na kipaji kikubwa cha kusakata kabumbu.

Mwenyewe amebainisha kuwa hajaenda KenGold kutafuta pesa, kwani angeweza kuzipata kwa kujiunga na timu zingine kubwa. Morrison hata kama yeye mwenyewe hajasema, lakini kila mmoja anajua kuwa anaweza kuichezea timu yoyote kubwa hapa nchini kutokana na uwezo wake.

Anasema ameamua kuichezea KenGold, kwa sababu anahitaji kucheza bila presha ili kujiweka sawa kimwili, na kiakili kwenye timu ambazo hazina mahitaji makubwa tofauti na angeenda timu nyingine, kwani ndiyo kwanza ametoka kwenye chumba cha majeruhi kujiuguza kutokana na majeraha aliyoyapata akiwa na Klabu ya FAR Rabat ya Morocco.

Akasema kuwa KenGold ipo ndani ya uwezo wake, kwani ni timu ambayo haiitaji mambo mengi zaidi ya kutaka kubaki tu Ligi Kuu, kitu ambacho anaweza kukifanikisha kwa kushirikiana na wachezaji wenzake.

Akiwa hapa nchini, Morrison alizichezea Klabu za Simba na Yanga, lakini kote huko amekuwa haishiwi na vituko, kiasi cha kuwa gumzo sana nje ya uwanja kuliko ndani.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa alikuwa akicheza vema mechi chache sana kwa uwezo wa hali ya juu kiasi cha kila mmoja kukubali uwezo na kipaji ambacho amejaaliwa kuwa nacho.

Kwa msimu mzima anaweza kuamua kucheza mechi tatu tu au nne kwa kiwango cha hali ya juu, lakini zingine zote akawa wa kawaida tu.

Na alifanya hivyo akiwa kwenye klabu kubwa zenye mashabiki wengi, hivyo wasiwasi wangu na baadhi ya mashabiki itakuwaje kwenye timu ndogo kama hiyo?

Kama alikuwa akiwapelekesha viongozi wa timu kubwa, viongozi wa KenGold wanaweza kumdhititi?

Wasiwasi wangu mwingine ni kwamba, KenGold, ambayo mbali ya kuwa ni ndogo, haipo Dar es Salaam, ambako ndiko hupenda zaidi kuishi, je anaweza kuishi Chunya bila kuomba ruhusa za mara kwa mara za kwenda Dar es Salaam?

Taarifa kutoka kwa watu wa Simba na Yanga zinasema, alikuwa na tabia ya kuondoka kambini wakati mwingine bila ruhusa, kitu ambacho kilikuwa kikiwakasirisha viongozi wa timu hizo na kushindwa kuishi naye kwenye mazingira kama hayo.

Labda kama mwenyewe ameamua kubadilika, kwani wakati mwingine muda ni mwalimu mzuri, inawezekana kabisa Morrison huyu siyo yule ambaye tunamfikiria na huenda amejifunza kutokana na makosa ya mwanzo na sasa ameamua kutulia.

Lakini kama atakuwa yule yule basi viongozi wa KenGold watafanya kazi ile ile ambayo ilikuwa ikiwakumba viongozi wa Simba na Yanga.

Inawezekana wao wakawa na dawa ya kumtuliza na kumfanya aelekeze nguvu zake uwanjani zaidi, pia uwezo wake uonekane kwenye michezo yote na si baadhi tu ambayo yeye mwenyewe inawezekana anaamua afanye kweli.

Kama Morrison akiamua kukipiga kweli na kuacha utukutu, hakuna winga yeyote nchini anaweza kufikia uwezo wake. Nafikiri pia kama Morrison akiwa kwenye kiwango kile ambacho kila mmoja anakifahamu, akiachana na 'utukutu', sidhani kama baada ya msimu ataendelea kuwa hapo.

Alijiunga na Yanga kipindi cha dirisha dogo la usajili 2020, na alipomaliza miezi yake sita, akatimkia Simba alipocheza kwa misimu miwili hadi 2022, akarejea tena Yanga, ambako alikipiga kwa msimu mmoja tu hadi 2023, akachukuliwa na aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, wakati huo, Nasreddine Nabi, kwenda katika timu aliyoenda kuifundisha, FAR Rabat ya Morocco.

**HABARI KITAIFA**

# TFS yaona fursa 'Mission 300'

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Misitu Tanzania (TFS) imesema kupitia 'Mission' 300 ya nchi za Afrika inayolenga kusambaza umeme kwa wananchi milioni 300 ifikapo mwaka 2030, zipo fursa nyingi ambazo zitapatikana ikiwamo kuimarisha sekta ya misitu na kuhifadhi mazingira.

Ofisa Utalii Mkuu na Mkuu wa Sehemu ya Utangazaji Utalii wa TFS, Anna Lawuo, alisema hayo wiki iliyopita wakati akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam baada ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika.

Alisema TFS ikiwa ni miongoni mwa taasisi za Serikali ya Tanzania ambazo zilishiriki mkutano huo, tayari imeona fursa nyingi ambazo kupitia mkakati huo wa nchi za Afrika, inakwenda kuchochea kufikiwa kwa lengo walilojiwekea la kurejesha uoto wa asili kiasi cha hekta milioni 5.2 ifikapo mwaka 2030.

"Sisi ni miongoni mwa taasisi za serikali ambazo zilishiriki katika mkutano huo kuonesha shughuli tunazozifanya kwa sababu unalenga kuwapatia umeme wananchi wa Afrika wapatao milioni 300 ifikapo mwaka 2030 na sisi tuna malengo yetu ambayo tumejiwekea ya kurejesha uoto wa asili kiasi cha hekta milioni 5.2 ifikapo mwaka 2030.

"Shughuli zetu sisi ni uhifadhi wa misitu, utalii na masuala ya nyuki na mkutano huo uligusa shughuli zetu moja kwa moja kwa sababu ukiangalia kwenye nishati safi ya umeme, inatumia sana nguzo za miti na sisi tunayo mashamba ambayo yanaotesha miti ambayo sisi kwetu ni fursa, tunaweza tukauza nguzo na miti yetu kwa wingi ambayo inasafirisha umeme.

"Lakini lengo letu kuu ni kuhifadhi mazingira ili kurejesha uoto wa asili ambao ulitoweka zamani na kama unavyojua Afrika na Tanzania tulitoa tamko la kurejesha uoto wa asili kiasi cha hekta milioni 5.2 ifikapo mwaka 2030.

"Lakini kutokana na uharibifu wa mazingira, uoto umetoweka. Kutokana na huu mkutano, utahamasisha zaidi watu wapande miti ili tupate uoto wa asili na hivyo kupata nishati kwa urahisi kwa sababu inategemea mazingira yaliyohifadhiwa," alisema. Alitolea mfano msitu wa Kalambo ulioko mkoani Rukwa, unatiririsha maji kwa sababu umehifadhiwa vizuri.

"Kwa hiyo moja kwa moja kupitia 'mission' hiyo, kwa TFS tutafaidika kwa sababu utaendelea kuhamasisha uhifadhi wa mazingira, tutauza nguzo za kusambazia wananchi umeme, utahamasisha uhifadhi wa mazingira, vyanzo vya maji na tutapata nishati safi."



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Immaculate Semesi (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu utupaji taka ambao hauathiri mazingira. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# NEMC yatoa tahadhari fukwe, miamba ya maziwa na mito mvua kubwa inayotarajiwa

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limewataka wananchi kuchukua tahadhari za kuepuka maeneo ya fukwe za bahari na miamba ya maziwa na mito ili kujinusuru na mafuriko na athari zake wakati ya mvua kubwa inayotarajiwa kunyesha hivi karibuni.

NEMC pia imezitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan Jiji la Dar es Salaam kuchukua hatua stahiki kupambana na watu wanaotupa taka ngumu katika mifumo ya maji na kuhakikisha mifumo hiyo ya maji inakuwa safi na kuimarisha njia na mikondo ya maji iwe safi wakati wote.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Immaculate Semesi alielekeza hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tahadhari ya mvua kubwa inayotarajiwa kuanza kunyesha.

Alisema ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha anaweka mazingira safi na salama ili kuepusha mafuriko na milipuko wa magonjwa ambayo yamekuwa yanarudisha nyuma jitihada katika ujenzi wa taifa.

Alisema taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) zilizotolewa Januari 23 mwaka huu, zimetabiri kuwapo mvua za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo ya mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Mara, Arusha, Kilimanjaro na Manyara.

**"(NEMC) inawatahadharisha wananchi kujiepusha kwa namna yoyote ile na vitendo vyenye kuchangia uharibifu wa mazingira kwa kuzingatia masuala kadhaa ikiwa**

Alisema taarifa hiyo ya TMA iliyataja maeneo ya mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro, Kigoma, Kagera, Geita, Mwanza na Shinyanga yanatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi juu ya wastani.

"(NEMC) inawatahadharisha wananchi kujiepusha kwa namna yoyote ile na vitendo vyenye kuchangia uharibifu wa mazingira kwa kuzingatia masuala kadhaa ikiwa pamoja na kuendelea kufuatilia kwa karibu taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na TMA ili kuwa na tahadhari ya maeneo yenye viashiria hatarishi," alisema.

Aliwataka wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya kandokando ya milima au miinuko mikali kuchukua tahadhari ili kuepukana na athari za maporomoko ya ardhi.

"Tunaomba Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuatilia kwa karibu maeneo ya uchimbaji madini na vifusi ili kuhakikisha jamii husika inakuwa salama na majanga yanayoweza kujitokeza kwenye maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha udhibiti wa taka ngumu ili zisizagae na kuingia katika mifereji ya maji ya mvua na mifumo ya majitaka na kusababisha kuziba," alisema.

Dk Semesi pia aliwataka abiria na wasimamizi wa vyombo vya usafiri kuwa na tahadhari wakati wa safari kwa kuzingatia kuwa maeneo ya barabara yanaweza kuwa yameathiriwa na mvua.

Alisema wananchi kwenye maeneo mbalimbali wanatakiwa kutoa taarifa kwa viongozi kwenye maeneo yao kuhusu athari zinazoweza kuwa zimejitokeza kutokana na hali hiyo.

"Wananchi wanakumbushwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, kifungu namba 57 na kuepuka ujenzi kwenye maeneo hatarishi ikiwa ni pamoja na maeneo ya kando ya mito, mabonde, fukwe za bahari na maeneo ya ardhi oevu.

"Kwa kuzingatia historia ya athari za mafuriko na maporomoko ya ardhi katika maeneo mbalimbali, ni muhimu kwa kila mmoja wetu kuwa makini na kuchukua tahadhari zinazohitajika ili kupunguza madhara yanayoweza kutokea kutokana na mvua hiyo," alisema.

# TCRA: Nusu ya wasafirishaji vifurushi wanakiuka kanuni

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema nusu ya watoa huduma za usafirishaji vifurushi nchini wanakiuka masharti ya kufikisha vitu vya wateja ndani ya siku moja kama ilivyoainishwa kwenye kanuni.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Mawasiliano Tanzania kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2024 iliyotolewa na TCRA, hakuna utekelezaji sahihi wa kanuni hizo.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari alisema mwishoni mwa wiki kuwa uchunguzi uliofanywa na mamlaka hiyo, umeonesha kuwa kati ya watoa huduma 17 waliofanyiwa tathmini, wanane ndio waliokidhi matakwa ya kanuni. Alisema TCRA ilipima ubora wa huduma za usafirishaji vifurushi ndani ya Tanzania kwa kuzingatia vigezo vya kanuni za ubora wa huduma hizo.

"Ukaguzi ulifanywa kwa watoa huduma za usafirishaji vifurushi wa Kanda A, yaani kati ya miji ya Arusha, Moshi, Tanga, Morogoro, Kibaha, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Iringa na Zanzibar.

Wanatakiwa wahakikishe kuwa angalau asilimia 85 ya vitu walivyopokea vinafika kunakotakiwa siku inayofuata," alisema mkurugenzi huyo.

Alisema kanuni hizo pia zina miji ya Kanda B ambamo wasafirishaji wanatakiwa kuhakikisha wanafikisha angalau asilimia 88 ya vitu wanavyopokea ndani ya siku tatu. Miji hiyo ni Tabora, Shinyanga, Kahama, Bariadi, Geita, Singida, Bukoba, Musoma, Kigoma, Mtwara, Lindi, Songea, Sumbawanga, Songwe, Mpanda, Babati, Njombe, Mkoani na Chakechake (Pemba).

"Watoa huduma kwenye kundi hili walikuwa na ufanisi zaidi. Kati ya 13 waliokaguliwa ni wanne tu wasiokidhi matakwa ya kanuni," alisema Dk. Bakari na kubainisha kuwa TCRA imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni hizo.

Alisema matokeo ya ukaguzi wa robo mwaka iliyoishia Septemba 2024, yalionesha kuwa watoa huduma 12 kati ya 19 wa kanda A hawakukidhi matakwa ya kanuni.

"Hadi Desemba 2024, TCRA ilikuwa imetoa leseni 153 za huduma za posta na usafirishaji vifurushi.

Kati ya hizo, moja ni ya Posta ya umma - Shirika la Posta Tanzania (TPC). Nyingine na idadi kwenye mabano ni usafirishaji kimataifa (6), Afrika Mashariki (2), ndani ya Tanzania (47), ndani ya miji (16), kati ya miji (79) na kulikuwa na jumla ya leseni 148 hadi Septemba 2024," alisema.

# Bilioni 2.9/- kujenga kiwanda cha kukamua mafuta ya pamba

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

SHILINGI bilioni 2.9 zinatarajiwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta yatokanayo na mbegu za pamba, kinachotarajiwa kuanza ujenzi wake mwezi huu katika mtaa na kata ya Mhongolo, Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga. Kiwanda hicho kinajengwa na Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).

Mwenyekiti wa KACU, Emmanuel Nyambi alibainisha hayo wakati wa kukabidhiwa magari mawili yenye thamani ya Sh. milioni 380 ambazo zinatokana na mkopo wa ujenzi wa kiwanda yatayotumika kubeba pamba. Hafla ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali, akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha.

Alisema kuwa katika msimu wa kilimo 2024/25, wamepokea mkopo wa Sh. bilioni 2.9 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta yanayotokana na mbegu za pamba ili kuongeza uzalishaji wake na ajira kwa vijana wanaowazunguka, uchumi wa wakulima kwa kulipa malipo ya pili na mapato ya serikali.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 1.159 zitatumika katika ujenzi wa kiwanda na usimikaji mitambo, Sh. bilioni 1.2 zitatumika kwenye ununuzi wa mitambo, Sh. milioni 142 ni gharama za ulipaji bandarini na Sh. milioni 380 zilizotumika katika kununua magari hayo ya kubeba zao hilo yenye uwezo wa kubeba tani 25 kila moja.

Mbunge wa Ushetu na Mwenyekiti mstafu wa chama hicho, Emmanuel Cherehani alisema kuwa ili kuongeza uzalishaji, wanatakiwa kuongeza maofisa ugani watakaowafikia wakulima na kuwakumbusha kununi 10 za kilimo na kupata pamba safi na bora itakayoshindana kwenye masoko ya kimataifa.

Ofisa Mikopo wa TADB, Andrew Ezekiel alisema wamekuwa wanakikopesha chama hicho fedha tangu msimu wa kilimo wa 2020/21 kwa mkopo wa Sh. bilioni 4.6 na walizitumia vyema katika lengo lililokusudiwa na kuurejesha kwa asilimia 100.

Alisema kuwa msimu huu wa 2024/25 wamewapatia mkopo wa Sh. bilioni 2.9 za ujenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta yanayotokana na mbegu za pamba na kuwataka kuutumia kwenye matumizi yaliyopangwa ili kitakapokamilika kilipe malipo ya pili kwa wakulima wake, ajira kwa vijana na kulipa zaidi mapato ya serikali.

Mkulima wa Msalala, Masumbuko Manga alisema watakuwa wanakiuzia chama hicho pamba ili kisikose malighafi na watakuwa na soko la uhakika kulinganisha na ilivyo hivi sasa, na malipo ya pili ambayo wamekuwa wanapokea kila mwaka yataongezeka na kuongeza uzalishaji na ushindani wa bei na kampuni zingine.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Macha, alisema katika moja ya kazi alizopewa na Rais Samia Suluhu Hassani ni kuinua zao la pamba, hivyo kiwanda hicho kitasaidia kuliibua upya zao hilo na malipo ya pili yanayolipwa ni njia mojawapo ya kuliinua zao kama yalivyo mengine ya biashara.

Aliwataka wakulima kuacha tabia ya kuzitelekeza kwa muda familia zao baada ya kuuza pamba badala yake washirikishe familia zao katika kupanga maisha ili kuondokana na umasikini katika kaya na kuhakikisha watoto wenye umri wa kwenda shuleni wanasoma.



Mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha akiongoza msafara wa ukaguzi wa zao la pamba na kusikiliza changamoto zinazowakabili wakulima, ili kuongeza uzalishaji katika kijiji cha Kisuke, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama mwishoni mwa wiki. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Kamati ya Bunge yapongeza ujenzi vituo vya kujazia gesi katika magari

**Na Halfani Chusi**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imepongeza serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa ujenzi wa mradi wa kituo mama cha gesi iliyoshindiliwa (CNG) na vituo vidogo viwili vya kupokea na kuhifadhi CNG kwa wateja wa awali.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, David Mathayo wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa kituo hicho cha kujazia gesi kinachojengwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) pamoja na kujionea maendeleo ya kituo cha kupokea gesi asilia cha Kinyerezi.

"Tunapongeza serikali kwa kupokea ushauri wa Bunge kwa kujenga kituo hiki kikubwa cha kujazia gesi kwenye magari ambacho kitasaidia vituo vingine vidogo kuchukua gesi katika kituo hiki ili kwenda kujaza gesi magari katika maeneo mengine," alisema.

Kamati hiyo ilishauri serikali kufikiria namna bora ya kusambaza miundombinu ya kusafirisha gesi ili kufika maeneo mengi nchini na kuendelea kuwapatia fursa wananchi kuendesha mitambo kwa kutumia gesi asilia badala ya mafuta kama ilivyozoeleka.

Mathayo alisema kusafirisha gesi kwa kutumia mtandao wa bomba ni nafuu zaidi kuliko kutumia magari na gesi inatakiwa kutumika mikoa yote kwa kuwa itapunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza mafuta kama dizeli na petroli.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga alisema sambamba na kituo hicho kutoa CNG kwa ajili ya kusambaza katika vituo vidogo ambavyo havijaunganishwa na miundombinu ya mabomba ya kusambaza gesi, kutakuwa na huduma ya kujaza CNG kwenye magari ya aina yote, yakiwamo malori, mabasi, magari madogo ya abiria na bajaji.

> **"Kituo kitaweza kuhudumia magari manane kwa wakati mmoja na kwa siku kitatoa huduma hii kwa magari 1,200 na hiki ndicho kituo chenye uwezo mkubwa kuliko vituo vyote vilivyomo nchini kwa sasa,"**

"Kituo kitaweza kuhudumia magari manane kwa wakati mmoja na kwa siku kitatoa huduma hii kwa magari 1,200 na hiki ndicho kituo chenye uwezo mkubwa kuliko vituo vyote vilivyomo nchini kwa sasa," alisema Judith.

Naibu Waziri huyo alisema gharama ya ujenzi wa mradi huo ni Sh. 18,946,766,486 ambazo zimegawanyika katika mikataba mitatu ya Mother station, Muhimbili station na Kairuki station na fedha zote zinagharamiwa na serikali kupitia TPDC.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Nishati inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa vituo vya kujaza gesi kwenye magari, jambo ambalo limepokewa vizuri kwa kuwa vituo hivyo vinaendelea kujengwa ili kuhakikisha huduma ya kujaza gesi kwenye magari inapatikana katika maeneo mbalimbali nchini kwa kuanza na mkoa wa Dar es Salaam.

Maulidi Malunga, dereva bajaji mkoani Dar es Salaam, alisema kujengwa kwa kituo cha kujaza gesi Tabata kumepunguza foleni katika vituo vingine vilivyokuwa Dar es Salaam.

"Tunaona watu wanaotumia gesi mwitikio ni mkubwa. Vituo vinapoongezwa inatia moyo, maana kuna kipindi mpaka watu walikata tamaa, ilikuwa tabu. Sasa tayari kuna vituo vingi vinajengwa kila kona, vikamilika kutakuwa hakuna tena usumbufu kupata huduma.

"Kwa sasa unaweza kupata huduma ya kujaza gesi kwenye gari au bajaji hapa Tabata. Kituo hiki kimesaidia kupunguza foleni kwenye vituo vya Ubungo, Tazara na Gongolamboto vilivyokuwapo awali," alisema.

Juma Karatu, dereva wa gari dogo la kubeba abiria, alisema kutokana na umuhimu wa gesi katika kutunza mazingira, hakuna budi kuongeza vituo vingi zaidi kama ambavyo jitihada zinaendelea Dar es Salaam, akishauri serikali iangalie namna ya kushusha gharama za gesi ili nao washushe gharama za usafiri (nauli) kuwapunguzia wananchi gharama za usafiri.

Janeth Michael, dereva wa gari la shule, alishauri vituo vya kujazia gesi vilivyopo na vinavyojengwa, viwe na mfumo wa umeme unaojigemea ili umeme unapokatika, huduma isisimame.

Alisema kuna vituo umeme ukikatika, huduma husitishwa, akisisitiza ni kikwazo kwa madereva.

Mchumi kutoka Taasisi ya Uongozi na Ujasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi alisema kuongezwa kwa vituo vya kujazia gesi katika vyombo vya moto kunapunguza mahitaji ya dola nchini.

"Vituo hivi vitapunguza mahitaji ya dola kwa sababu ile fedha ya kigeni ambayo ingetumika kununua mafuta, itaokolewa. Kwa sasa moja ya maeneo yanayotumia fedha nyingi za kigeni ni uagizaji mafuta. Kama gesi ikitumika, maana yake unaokoa matumizia ya fedha za kigeni, jambo ambalo litasaidia kukuza mzunguko wa fedha za ndani.

"Dola tunaipata kwa kuuza vitu nje ya nchi, au kwa kukopa. Tukishahamia kwenye matumizi ya gesi inayozalishwa nchini, matumizi ya dola yatapungua, hatua hii ina faida nyingi kiuchumi," alifafanua Dk. Olomi.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, mpango wa serikali ni kuwa vituo 15 vya kujazia gesi. Hivi sasa tayari kuna vituo saba mkoani Dar es Salaam; vinne vinafanya kazi na vitatu viko katika hatua ya mwisho ya ujenzi wake.



# Mzava kuanza na watendaji wenye majibu jeuri

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Wilaya Moshi mkoani Kilimanjaro, Godfrey Mzava, amesema atakuwa mkali kwa watendaji watakaoshindwa kusimamia miradi ya maendeleo.

Amesema pia hatawafumbia macho watendaji wanaotoa majibu yasiyofaa kwa wananchi na watakaoshindwa kutoa majibu ya changamoto za wananchi.

Mzava, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kuingia kwa mara ya kwanza ofisini kwake.

Alisema vitendo hivyo havivumiliki na kuwaagiza wakurugenzi kuendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu wa watendaji ili wananchi waweze kupata haki.

"Wakurugenzi fanyeni ufuatiliaji mzuri wa wa watendaji katika idara zenu, wananchi waweze kupata haki kwa wakati. Thamani ya pesa iendane na uhalisia, hatutawafumbia macho wala kuwaonea, hivyo niombe tusaidiane kuleta majawabu,"alisema.

Alisema jambo lingine limeonekana kudorora kwa uwajibikaji hasa kwa vijana na kujikita katika matumizi ya pombe kupitiliza jambo ambalo tutalifanyia kazi.

"Moshi inasikika kwa matumizi ya pombe kupindukia, kupitia wataalamu wangu, tutakwenda kutafuta chanzo cha matatizo hayo na kuwalekeza katika ufanyaji wa kazi kwa kuzingatia mikopo ya halmashauri ili kuwa wabunifu na kukuza kipato cha mtu moja mmoja na taifa kwa ujumla,"alisema.

Baadhi ya wananchi wilayani Moshi akiwemo Julieth Lewis alisema ikiwa wananchi wanapata majawabu ya kero zinazowasibu wataweza kujikita katika shughuli za maendeleo.

# Mradi wa maji kumaliza kero, magonjwa ya mlipuko

**Na Beatrice Shayo,** MANYARA

WANANCHI wilayani Hanang' mkoani Manyara, wanatarajia kunufaika na mradi wa maji utakaowaondolea magonjwa ya milipuko yanayotokana na uchafu wa mazingira na vyanzo vya maji.

Mradi huo unatekelezwa na Shirika la WaterAid la Uingereza kwa kushirikiana na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) mkoani Manyara.

Akizungumza katika mkutano wa ushirikishwaji wa wadau mjini Katesh, Mkuu wa miradi wa Water Aid Tanzania, Beda Levira alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu.

Levira alisema WaterAid katika kutekeleza mradi wa mfano Hanang' utatatua changamoto ya maji safi, vyoo bora na usafi wa mazingira na utanufaisha wakazi wengi wa vijiji 96 wa kata 33.

"Watu watapata maji kwa asilimia 100 na kuondokana na changamoto ya magonjwa ambukizi yanayotokana na uchafuzi wa mazingira na vyanzo vya maji," alisema Levira.

Mhandisi wa maji kutoka RUWASA, Barnabas Taligunga, alisema mradi huo utaongeza nguvu ya uboreshaji wa usafi wa miundombinu ya kusambaza maji kutoka kwenye vyanzo hadi kwa watumiaji ili kudhibiti uwezekano wa kusambaa magonjwa kipitia maji.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Dk. Andrew Method alitoa wito kwa viongozi wa Hanang' kutoa ushirikiano kwa maofisa wa WaterAid katika kutekeleza mradi huo ili uwe mfano kwa wilaya nyingine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Programu za Kimataifa (IPD), WaterAid UK, Amaka Godfrey, alisema watashirikiana na serikali kuhakikisha mradi huo unawanufaisha wananchi wengi.

Alisema mbinu iliyotumika ya kuifikia wilaya hiyo katika upatikanaji wa maji ni jambo zuri na imekuwa ikifanya vizuri katika nchi nyingine.

Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Hanang' walisema kuwa wataulinda mradi huo ili uweze kuwanufaisha wao na kizazi kijacho.

# Wakulima wang'oa mazao kisa ugonjwa wa BBTV

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

> "Mpaka sasa tuna wakulima 197 waliong'oa migomba yote kuteketeza mashamba yao ili kuua virusi hivyo vinavyosababisha ugonjwa wa BBTV; ambao wamenufaika na miche mipya na ya kisasa.

WAKULIMA wa ndizi katika mikoa ya Kigoma na Mbeya, wameteketeza mazalia ya zao hilo shambani, ili kuudhibiti ugonjwa wa fungashada la migomba (BBTV) usiendelee kusambaa na kuhatarisha zaidi usalama wa chakula.

Ugonjwa huo umeacha maumivu kwa wananchi wanaolima na kutegemea kilimo cha ndizi, kwa ajili ya chakula na biashara.

Akizungumza katika kikao kazi kilichomalizika juzi katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro, kwa ajili ya kuandaa rasimu ya mkakati na mpango kazi wa kutokomeza ugonjwa huo, Ofisa Kilimo kutoka Sekta Binafsi, Plant Village Tanzania, Joachim Gobanya alisema:

"Mpaka sasa tuna wakulima 197 waliong'oa migomba yote na kuteketeza mashamba yao ili kuua virusi hivyo vinavyosababisha ugonjwa wa BBTV; ambao wamenufaika na miche mipya na ya kisasa.

Jumla ya ekari mpya za uzalishaji wa ndizi zilizoanzishwa, ni 203 na idadi ya miche ambayo imeshasambazwa tangu msimu wa 2023/2024 na msimu wa 2024/2025, ni 160,000. Ambayo miche hiyo kuna aina ya mzuzu, kimalindi, talibani 4 FIA 23 na asiankara."

Alipoulizwa kuhusiana na ugonjwa huo, Mtaalamu wa Utafiti wa Visumbufu vya Mimea na Udhibiti wa Chuo Kikuu cha Kilimo Cha Sokoine (SUA), Prof. Gration Rwegasira, alisema mpaka sasa SUA imesaidia suala hilo kwa kutoa wataalamu na kuwapeleka mikoa ya Kigoma na Mbeya kuwafundisha wakulima na kuwaanzishia maabara, kwa ajili ya utafiti wa ugonjwa huo.

Mshauri wa kiufundi (ulinzi wa mimea) wa Shirika la Chakula Duniani (FAO), Dk. Monday Ahonsi, akieleza umuhimu wa kutokomeza BBTV Tanzania, ubia na jukumu la STREPHIT katika mchakato huo, alisema FAO kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), limesisitiza dhamira yake ya kutokomeza ugonjwa huo kupitia mradi wa kuleta mabadiliko wa STREPHIT.

Alisema: "Mpango huu unalenga kuimarisha huduma za afya ya mimea na kukuza upatikanaji wa mazao ya kilimo yaliyo salama, yenye ubora wa juu, ndani na nje ya nchi.

"BBTV ni tishio kubwa kwa uzalishaji wa ndizi, zao kuu kwa mamilioni ya Watanzania. FAO inasalia na nia ya kufanya kazi na washirika wa ndani na kimataifa ili kufikia kutokomeza kabisa kwa BBTV, kukuza mustakabali wa kilimo wenye afya na ustahimilivu zaidi kwa Tanzania."




Mthaminishaji wa madini ya vito, Seleman Hamis (wapili kushoto), akizindua mnada wa madini ya Tanzanite ya kampuni ya Chusa Mining Ltd, katika mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Dawa za kulevya kilo 204 zateketezwa Muriet

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Kanda ya Kaskazini, imeteketeza kilogramu 204.8 za dawa za kulevya katika dampo la Muriet lililopo Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Katika idadi hiyo zilizoteketezwa, mirungi ilikuwa ni kilogramu 172.8165 na bangi kavu ilikuwa kilogramu 32.0.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa mwishoni mwa wiki na DCEA, Ofisa wa Kanda hiyo, Innocent Masangula, alisema kati ya watuhumiwa waliokamatwa wakiwa na dawa hizo, wamo wanaume 25 na wanawake wanane.

Aidha, alisema watuhumiwa wote walikamatwa katika operesheni zilizofanyika kuanzia Januari 2024 hadi Januari 27, 2025 katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara.

Matukio ya dawa hizo, zimewahusisha watuhumiwa 33 waliokamatwa kwa makosa ya kupatikana na dawa hizo.

Hata hivyo, alisema taratibu za uteketezaji wa vielelezo hivyo zimefanyika kwa kuzingatia sheria na miongozo husika na Mahakama ya Wilaya ya Arusha, iliridhia vielelezo hivyo viteketezwe kwa kuwa vikikaa muda mrefu vinaweza kupoteza uhalisia na hata kupelekea kuharibika.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa watuhumiwa saba miongoni mwa 33 waliokamatwa na dawa hizo, tayari kesi zao zilishatolewa hukumu za vifungo mwaka 2024.

Pia, kesi nyingine zinaendelea katika mahakama za ngazi ya mikoa na wilaya katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara.

Wahusika walioshiriki katika shughuli ya uteketezaji wa dawa hizo ni kutoka taasisi za serikali zilizopo mkoani Arusha, mwendesha mashtaka kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mkoa wa Arusha, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kanda ya Kaskazini, Hakimu Mkazi Mwandamizi Mahakama ya Arusha na Ofisa Mazingira Halmashauri ya Jiji la Arusha.

# Shule jirani na nyumbani yaongeza mahudhurio ya wanafunzi

## -Ni iliyojengwa na TASAF; mimba, ndoa za utotoni...

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

SERIKALI kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) imejenga madarasa mapya katika Shule ya Sekondari Igogwe wilayani Ilemela na kurahisisha upatikanaji elimu karibu na jamii.

Imeelezwa kuwa hatua hiyo imetatua kero ya umbali mrefu waliokuwa wanatembea baadhi ya wanafunzi kila siku kwenda shuleni na kurudi nyumbani, hata wengi wao kuwa watoro na kutumbukia katika mimba na ndoa za utotoni.

Edina Julius, mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 2022, ni mmoja wa wanafunzi waliopata adha ya kutembea umbali mrefu kuisaka elimu. Anaeleza furaha yake na matarajio ya ndoto zake zinaelekea kutimia baada ya kupata nafasi ya kuhamia katika shule hiyo iliyoko jirani na nyumbani kwao.

Anasema hatua hiyo imewanusuru wanafunzi waliokuwa wanatembea umbali wa kilomita 10 kila siku, na sasa wananufaika na madarasa yaliyoko karibu na nyumbani, hivyo kuwa na mahudhurio mazuri shuleni, bidii darasani na mafanikio ya kitaaluma.

Anasema kuwa awali alikuwa analazimika kutembea umbali mrefu kwenda Shule ya Sekondari Kisunda na alikumbana na vikwazo vingi njiani, akivitaja vilihatarisha mwenendo wake kimasomo. Kuhamia shule jirani na nyumbani kwao ni nuru iliyoondoa kiza kilichotishia ndoto zake kielimu.

Abdalah Shabani, mwanafunzi wa shule hiyo, anaeleza kuwa awali alikuwa anatembea umbali mrefu na alifika shuleni akiwa amechoka, hivyo kushindwa kumsikiliza vizuri mwalimu darasani.

"Ndani ya wiki moja unakuta mtu anakwenda shuleni kwa siku tatu kutokana na mwili kuchoka kwa safari za nenda rudi kwa miguu. Hapo lazima uwe mtoro, unakuwa unakosa masomo.

"Baada ya shule hii kujengwa tuliomba nafasi za kuhamia hapa tukapata, kwa kweli hata kwenye masomo tunafanya vizuri, tunaishukuru serikali, wadau wa maendeleo na TASAF kwa kushirikiana kutujengea shule hii. Pia pongezi nyingine tuwape walimu wetu ambao wanajitahidi kutufundisha," anasema mwanafunzi huyo.

Diana Devidi, mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule hiyo, anaungana na wenzake na kueleza wanavyonufaika na miundombinu mbalimbali iliyoko shuleni huko, ikiwamo mradi wa maji na umeme. Wanasoma hadi usiku pasina kikwazo chochote kutokana mazingira rafiki yaliyoko shuleni huko.



Mwonekano wa majengo ya Shule ya Sekondari Igogwe, wilayani Ilemela iliyojengwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

Mmoja wa wazazi wa watoto wanaoishi jirani na shule hiyo, Amina Abdul, anasema kuwa awali hawakuwa na shule ya sekondari, hivyo kuwalazimu wanafunzi kutembea umbali mrefu uliochangia watoto wa kike kukutana na vishawishi vilivyochangia mimba za utotoni.

"Vishawishi vilikuwa vingi, hasa bodaboda. Walikuwa wanawaharibu watoto wetu kwa kuwadanganyia 'lifti', wengi walikatisha masomo kwa mimba," Amina anasimulia kilichokuwa kinajiri.

Kauli ya mzazi huyo inaungwa mkono na Diwani William Mashamba ambaye anaeleza kuwa ukanda huo haukuwa na shule yoyote ya sekondari, hivyo TASAF imesaidia upatikanaji shule nzuri na ya kisasa.

"Watoto walikuwa wanakwenda kutafuta elimu kwa kutembea kilomita 10 kwenda kusoma. Ninajua mkurugenzi umesoma masomo ya sayansi. Kwa kutembea umbali huo, nina imani utakuwa umepoteza unachojifunza, lakini serikali kwa kushirikiana na wadau wameyakabili matatizo yetu na kutuletea shule," anasema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Igogwe, Athanas Manyika anasema shule ilijengwa mwaka 2022, ikianza na madarasa manne ambayo yalijengwa na wananchi kwa kushirikiana na halmashauri na baadaye TASAF iliongeza nguvu na kujenga miundombinu ambayo imekidhi mahitaji ya wanafunzi.

"Elimu ilikuwa 'nzito' kutokana na umbali, lakini sasa hivi watoto wengi waliokuwa hawaendi kuripoti shuleni, wanakuja kuripoti huku kwa kuwa kuna miumdombinu ya kutosha na mazingira mazuri ya kujifunzia tofauti na maeneo mengine.

"Hapa tuna maktaba, maabara, mabweni, madarasa na jengo la utawala. Wanafunzi wanafanya vizuri katika masomo yao kwa sasa. Imeondoa changamoto ya kuacha shule na kupata vishawishi njiani. Hivi sasa shule imo katika mtaa wao na wanakuja kwa wingi," anasema.

Japhet Boaz, Mkurugenzi wa Mifumo, Tathmini na Mawasiliano TASAF Makao Makuu Dodoma, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, anasema wamekuwa wanatekeleza miradi mingi nchini kwa lengo la kupunguza au kuondoa umasikini kwa wananchi ambao walikuwa na hali duni. Moja ya miradi hiyo ni ujenzi wa shule hiyo.

Boaz anasema ujenzi wa shule hiyo umetatua kero ya umbali mrefu waliokuwa wanatembea wanafunzi wa maeneo hayo.

"Hiyo ilikuwa ni changamoto ukizingatia jamii zetu ni za kimaskini, mwanafunzi angelazimika kutembea kwa miguu kwenda na kurudi au kwa kutumia baiskeli, Ujenzi wa miradi kama hii umesaidia wanafunzi kutumia muda ambao wangeupoteza barabarani, kukaa darasani na kusoma. Ni matamanio ya serikali kuwa na kizazi kilichoelimika kinachoweza kufikia malengo yake," anasema.

Meneja wa Miradi ya TASAF, Paul Kijazi anasema mradi huo ulianza mwaka 2022 na ni miongoni mwa miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta kwa Wingi Duniani (OPEC).

Kijazi anasema wanayo miradi 12 ambayo inagawanyika katika sehemu kuu saba; maabara mbili, madarasa manne, matundu ya vyoo 12, bweni la wasichana na wavulana, maktaba ya kusomea, nyumba mbili za walimu na jengo la utawala.

Anaeleza kuwa mradi huo unagharimu Sh. milioni 891 pamoja na nguvu ya wananchi kwa sababu katika miradi yao utaratibu wao jamii inapaswa kushiriki kwa kuchangia asilimia 10 ambayo si lazima itolewe fedha, bali inaweza kutolewa kwa michango ya aina mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kushiriki katika kazi kama kuchimba msingi, kusafisha eneo, kuchota maji na kusogeza matofali.

"Miundombinu ya maji ni sehemu ya mradi ambapo tumefanikisha kupatikana maji kutoka sehemu ambayo ilikuwa ya mbali hadi eneo hili la shule, hapo awali shule haikuwa na miundombinu ya kuleta maji mpaka hapa, sasa hivi maji yanapatikana na yanaingia sehemu mbalimbali za shule," anasema Kijazi.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Ilemela, Gasper Makelemo anasema miradi hiyo ni maendeleo ya wananchi, hivyo wananchi wawe tayari kuisimamia na ikamilike kwa wakati na kupata matokeo yenye tija ndani ya jamii.

Mtaalam wa Hifadhi ya Jamii kutoka Benki ya Dunia (WB), Tumainiel Ngowi anasema wameridhika kwa kiasi kikubwa baada ya kuona jitihada zilizofanywa katika kuboresha maisha ya wanufaika wa TASAF na hiyo inawapa moyo na motisha kuendelea kupigana vita na umasikini katika kaya husika.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na lile la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) yanautaja umbali kutoka nyumbani hadi shuleni ni moja ya changamoto zinazochangia kukwamisha malengo ya wasichana wengi kielimu hususani katika nchi nyingi zinazoendelea na ni sehemu ya vyanzo vya utoro, mimba za utotoni, ndoa za utotoni na ufaulu duni.

Takwimu za UNICEF za mwaka 2012 ziliitaja mikoa inayoongoza kwa ndoa za utotoni nchini, Mwanza ikishika nafasi ya 10 kwa kuwa na asilimia 37. Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa asilimia 59, ukifuatwa na Tabora asilimia 58, Mara asilimia 55, Dodoma asilimia 51 na Lindi asilimia 48.

Vilevile, Shirika la Afya Duniani (WHO) katika utafiti uliochapishwa mnamo Januari 2016, liliitaja Tanzania kuwa nchi ya tatu barani Afrika kwa matukio ya ndoa na mimba za utotoni kwa asilimia 28.



Nipashe
Spotika



TEAM RAIOLA NA MIKOBA YA MINO RAIOLA UWAKALA WA WACHEZAJI UK. 12



MARTIN ODEGAARD

# USAJILI WA WACHEZAJI WA5 BORA WA ARSENAL JANUARI

**LONDON, England**

ARSENAL mara nyingi imekuwa na nguvu ya kuvutia inayohitajika kusajili wanasoka wenye vipaji na wa kutumainiwa zaidi duniani, lakini wachezaji wake wengi wa kustaajabisha wamekuja wakati wa dirisha la majira ya joto.

'Washikabunduki' hao hawajawahi kuwa na matumizi makubwa ya fedha kwa usajili wa Januari na rekodi yao katika soko la majira hayo ya baridi ni mchanganyiko.

Wachezaji wachache wakubwa walisajiliwa Kaskazini mwa London Januari, lakini kumekuwa na hadithi kadhaa za mafanikio zinazojulikana na za mabadiliko.

Makala haya inaangalia usajili bora wa muda wote wa Arsenal katika kipindi cha Januari tangu dirisha hilo la majira ya baridi lilipoanzishwa rasmi kwa mara ya kwanza wakati wa msimu wa 2002/03.

**5. Nacho Monreal**

Ingawa mbali na Arsenal kuongeza uzuri zaidi enzi za Ligi Kuu England, wachache wamefanya kazi ngumu zaidi wakiwa wamevalia jezi nyekundu kuliko Nacho Monreal. Alipowasili kwa pauni milioni 8.5 kutoka Malaga mwaka 2013, aliendelea kukaa miaka sita na nusu akiwa na Washikabunduki hao, na alicheza zaidi ya mechi 250 na kushinda mataji matatu ya FA.

Beki huyo wa kushoto alikuwa mtumishi asiyechoka wakati wa kipindi kigumu kwa klabu hiyo, akivaa moyo wake kwenye mkono wake na kucheza zaidi ya mechi 35 katika kila msimu wake kamili. Aliondoka Emirates kama kipenzi kikuu cha mashabiki.

**4. Emmanuel Adebayor**

Emmanuel Adebayor na Arsenal hawakumalizana kwa maelewano mazuri. Baada ya kuondoka Kaskazini mwa London kuelekea Manchester City mwaka 2009.

Kukimbia kwa urefu wa uwanja na kupiga magoti mbele ya mashabiki wa Arsenal hakukuwa na uwezekano wa kupendwa na mashabiki wake, lakini mchezaji huyo wa Kimataifa wa Togo bado alikuwa usajili wa kuvutia alipojiunga na Washikabunduki hao mwaka 2006.

Alifunga mabao manne ya Ligi Kuu England katika kipindi chake cha kwanza cha nusu msimu na akafanikiwa kuongeza idadi hiyo mara mbili katika kampeni iliyofuata. Lakini ilikuwa wakati wa msimu wa 2007/08 ambapo alivutia sana, akifunga mabao 24 kwenye ligi katika mechi 36.

3. Theo Walcott

Theo Walcott aliipa Arsenal miaka 12 ya utumishi wa kutegemewa na wa kujitolea, na kuingiza jina lake katika vitabu vya historia ya klabu hiyo baada ya kuhamia London Kaskazini kutoka Southampton mwaka 2006. Hakuchukua muda mrefu kuongeza kasi ikizingatiwa alisajiliwa akiwa na umri wa miaka 16 pekee.

Winga huyo mwenye kasi aliichezea Arsenal mechi 382, akiifungia klabu hiyo mara 106, huku kampeni yake nzuri zaidi ikiwa ni ile ya msimu wa 2012/13. Alitikisa nyavu mara 21 na kutoa pasi 11 za mabao katika mashindano yote, na kuongeza jumla ya mabao 23 kutoka msimu uliofuata.

Ingawa zawadi ya mataji haikupatikana sana wakati wa uchezaji wake akiwa na Arsenal, Walcott alitwaa Kombe la FA mara mbili tofauti, hata kufunga katika fainali ya msimu wa 2014/15 wakati wa ushindi wa 4-0 dhidi ya Aston Villa.

**2. Pierre-Emerick Aubameyang**

Pierre-Emerick Aubameyang ndiye mchezaji aliyevunja rekodi ya Arsenal msimu wa 2017/18, akijiunga na klabu hiyo kwa pauni milioni 56. Matarajio yalikuwa juu sana kwa mshambuliaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, ambaye alikuwa maarufu kwa ukatili wake mbele ya lango na kasi ya ajabu.

Tabia hizo zilionekana haraka pale Emirates alipofunga mabao 14 na kusaidia katika mechi nyingi katika miezi sita yake ya kwanza. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Gabon, aliboresha idadi hiyo msimu uliofuata, na kutwaa Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England kwa kufunga mabao 22.

Mabao hayakukauka katika kampeni zilizofuata na bao lao la kwanza kwa wakati muafaka ni katika fainali ya Kombe la FA msimu wa 2019/20 dhidi ya Chelsea ambalo liliihakikishia Arsenal ushindi.

Mzozo kati yake na kocha Mikel Arteta ulisababisha maisha yake ya soka ya Arsenal kuisha mapema, lakini anabakia kuwa mmoja wa wababe wa siku hizi wa klabu hiyo.

**1. Martin Odegaard**

Arsenal ilimsajili Martin Odegaard kwa mkataba wa kudumu wakati wa dirisha la majira ya joto, lakini awali alikuwa amejiunga na klabu hiyo kwa mkopo wa miezi sita Januari 2021.

Akiwa ametajwa kuwa nyota katika umri mdogo sana, uwezo wa Odegaard haukutosha kumhakikishia kucheza katika kikosi cha kwanza kule Real Madrid licha ya kucheza kwa mkopo mara kadhaa. Uhamisho wa muda kwenda Emirates ulimfanya kuinua mchezo wake na wababe hao wa Hispania walikuwa na furaha kuidhinisha dili la pauni milioni 30.

Odegaard amekuwa mtu wa mabadiliko katika chumba cha injini kwa Arsenal, akiongoza mapinduzi ya klabu chini ya Arteta. Sasa akiwa nahodha, ustadi wake, ubunifu na mguu wa kushoto umewasukuma Washikabunduki hao kwenye kilele cha ukuu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ana muda mwingi wa kupambana zaidi kuacha urithi wake Arsenal.

## ISIKUPITE

MABAO mawili aliyofunga Mohamed Salah juzi wakati Liverpool ikishinda 2-0 dhidi ya Bournemouth, yanamfanya kufikisha mabao 178 kwenye Ligi Kuu England na kuwa katika nafasi ya sita ya wafungaji bora kwenye historia ya zama za Premier League akiwa na bao moja mbele ya Frank Lampard mwenye 177. Pia sasa Liverpool haijapoteza mechi hata moja katika michezo 19 ya ligi hiyo, tangu walipofungwa bao 1-0 nyumbani na Nottingham Forest mnamo Septemba 14, mwaka jana, huku Bournemouth, huo ukiwa mchezo wao wa kwanza kupoteza katika mechi 12 za ligi.



# TEAM RAIOLA NA MIKOBA YA MINO RAIOLA UWAKALA WA WACHEZAJI



JUSTIN KLUIVERT

**MILAN, Italia**

WAKALA bora, Mino Raiola, na ulimwengu wa uhamisho wa wachezaji wa soka ulikuwa unaenda naye sambamba.

Raiola pengine alikuwa wakala mashuhuri zaidi kuliko wote, mwenye sifa ya kutisha ya kufanya mazungumzo ya juu zaidi kwa ajili yake na wateja wake.

Wasifu wake ulikosolewa na makocha wawili tu maarufu, Sir Alex Ferguson na Pep Guardiola.

Lakini kifo chake mwaka 2022 kilitarajiwa kuangusha himaya ya uhamisho ambayo Raiola alikuwa ameijenga kwa miaka mingi.

Binamu yake, Enzo anashiriki kumbukumbu yake anayemtaja kama "onesho la mtu mmoja" na anaelezea jinsi urithi wa Mino unavyoendelea.

Kujijenga upya katikati ya huzuni

"Kifo chake hakikutarajiwa kabisa," anasema Enzo Raiola katika mahojiao na BBC Sport.

"Hata alipokuwa mgonjwa, umakini wetu wote ulikuwa kumsaidia kupata nafuu.

"Hakuna kitu kilikuwa mahali, na hatukufikiria tungehitaji kupanga upya kila kitu huku tukiwa na huzuni - ilikuwa ngumu sana."

Mino alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 54 huko Milan Aprili 2022, na alipata heshima na rambirambi nyingi kutoka ulimwenguni kote.

Mshambulizi wa Manchester City, Erling Haaland alimwita "wakala bora zaidi", fowadi wa Italia, Mario Balotelli alisema alikuwa "baba yangu wa pili" na Zlatan Ibrahimovic alisema "nililia sana hadi tone langu la mwisho."

Lakini familia ya Raiola ililazimika kusonga mbele haraka au kuhatarisha kupoteza biashara ya Mino, ambayo ilianzishwa kwa uhamisho wa kwanza wa Pavel Nedved na Dennis Bergkamp na baadaye ikaonesha hatua kubwa kwa Haaland na Paul Pogba.

Hivyo ndivyo, vyombo vya habari vya kimataifa vilivutiwa na Raiola, kulikuwa na ripoti za uwongo za kifo chake alipokuwa bado anapigania uhai wake.

"Tulikuwa na wachezaji wetu na vyombo vya habari vikiuliza hali yake - wakati mawakala wengine katika makampuni pinzani walijaribu kuiba wachezaji wetu," anasema Enzo.

"Ilitubidi tujipange upya na kuitikia kila kitu. Wakati wote nilipokuwa nikienda hospitalini kwa dakika za mwisho za Mino nilikuwa na woga wa kumpoteza.

"Nilikuwa nae kwa miaka 15. Mino alikuwa msukumo, baada ya kufanya kazi kwa zaidi ya siku 30. Alikuwa onesho la mtu mmoja. Lakini hatukuweza kuacha kazi yake ipotee na ilibidi tujenge upya himaya yake."

Kifo kilibadili mambo

Wakati baadhi ya wachezaji wakubwa waliungana na mshirika wa zamani wa Raiola wa kibiashara Rafaela Pimenta, wengine walienda na Enzo - pamoja na skauti aliyeaminika zaidi wa Mino, Jose Fortes Rodriguez - katika operesheni iliyojengwa upya iliyopewa jina la Team Raiola.

"Mino hangeruhusu mtu yeyote kumkanyaga," anakumbuka Enzo. "Angepigana katika mazungumzo, au hata kwenye ukumbi wa hoteli ili kupata chumba sahihi.

"Alikuwa na pande mbili tofauti kwa utu wake. Katika mahojiano na mazungumzo, alionekana kuwa na ushindani mkali.

"Bado nyuma ya pazia na wachezaji wake na washirika anaweza kuonesha hisia kubwa ya huruma na ubinadamu.

"Mimi na Jose tunapenda kuingia ulingoni kuwalinda wachezaji wetu pia, lakini bado hatujazungumza waziwazi kwenye vyombo vya habari."

Kuangalia kizazi kipya

Raiola alikuwa ameona orodha ndefu ya wateja ikija na kuondoka, baada ya kuhusika katika mikataba ya uhamisho wa Romelu Lukaku, Marcus Thuram, Matthijs de Ligt, Noussair Mazraoui na Denzel Dumfries.

Raiola alipoanza kutoka katika maisha duni kwenye biashara ya mgahawa wa familia ya pizza huko Haarlem, karibu na Amsterdam, Enzo aliingia kwenye soka akiwa anaendesha karakana ya magari ya familia karibu na mji wa Naples.

Hatimaye alijiunga na binamu yake katika soka wakati wa uhamisho wa Ibrahimovic mwaka 2006 kutoka Juventus kwenda Inter Milan, akimsaidia Raiola kumhamisha mteja wake kutoka kwa wababe wa Turin walioshuka daraja wakati wa kashfa ya upangaji matokeo.

Timu iliyobadilishwa umbo la Raiola pia inawakilisha baadhi ya vipaji vinavyoongoza katika Ligi Kuu England - ikiwa ni pamoja na Micky van de Ven wa Tottenham Hotspur, Ryan Gravenberch wa Liverpool na Justin Kluivert wa Bournemouth.

Ili kuendana na matarajio ya kizazi kipya, Team Raiola hutumia kampuni tofauti inayoendeshwa na mtoto wa Raiola, Mario ambayo inajishughulisha na uchanganuzi wa data, haki za vyombo vya habari, udhamini wa chapa, mitandao ya kijamii na mawasiliano.

"Tunataka tu wachezaji 11 wa juu katika soko letu kudumisha mwingiliano kama familia," anasema Enzo.

"Lakini lazima pia tusiwe bendi ya mtu mmoja kama iliyokuwa hapo awali.

"Tunapoenda kwa klabu kufanya mazungumzo, wana silaha na data - unapaswa tu kuangalia jinsi Brentford na Brighton wanavyofanya kazi. Data inatumika kuchunguza kizazi chetu kijacho, katika maeneo ambayo tuna maskauti wachache."

Rodriguez - skauti wa muda mrefu aliyegeuka wakala wa Raiola - anashiriki mawazo fulani juu ya wateja wake watatu wa Ligi Kuu England.

Micky van de Ven

"Raiola alinipigia simu na kusema 'nimeona mchezaji mzuri sana katika Daraja la Pili Uholanzi huko Volendam'. Nikasema 'Hiki si kiwango cha wachezaji tunachoangalia', lakini Mino alisisitiza niangalie.

"Nilikuwa nimesikia hadithi kuhusu Van de Ven. Nilimpigia simu Mino baada ya dakika 20. Ilinichukua muda mrefu kuona vya kutosha kuhusu kasi na ujasiri aliokuwa akicheza nao.

"Wakati huo, nilimwambia Mino 'Tunahitaji kumchukua mchezaji huyu'. Siku zote nilikuwa nikifikiria anaweza kucheza Ligi Kuu England kwani ana nguvu kiakili na kimwili."

Ryan Gravenberch

"Nilipomuona Ajax kwa mara ya kwanza nilipenda sana kipaji chake.

"Nilikuwa kama 'Wow, wow, wow'. Alipokuwa na umri wa miaka 14 au 15 niliendelea kumwambia anaweza kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani.

"Bado anahitaji kuimarika kwa sasa kwa sababu Ryan ni mmoja wa wachezaji wanaohitaji kujionesha zaidi, ni mstaarabu sana uwanjani."

Justin Kluivert

"Nilimwona alipokuwa mdogo na tayari katika kikosi cha kwanza cha Ajax. Kila mtu aliona kuwa ana kazi kubwa mbele yake. Alikuwa mtu mkubwa.

"Amecheza ligi zote bora Ulaya na yuko Bournemouth, akitengeneza mabao.

"Nina furaha sana kwa Justin kwamba anaweza kufanya hivi katika kiwango hiki cha Ligi Kuu, lakini amekuwa akifanya hivyo tangu akiwa kijana mdogo."

## Nukuu

"Kila mtu anamtaka, ikiwa ni pamoja na sisi - tunataka aongeze [mkataba], bila shaka. Hilo liko wazi," **Kocha wa Liverpool, Arne Slot, kuhusu mustakabali wa Mohamed Salah kusaini mkataba mpya wakati huu wa sasa ukimalizika mwishoni mwa msimu huu.**



"Hakika sielewi. Baada ya sekunde nane, nilikuwa nikifikiria 'wema wangu hii ni nzuri sana'", **Kocha wa Everton, David Moyes, akizungumzia bao lililofungwa na Abdoulaye Doucoure katika sekunde ya 10, wakati wakishinda 4-0 dhidi ya Leicester City kwenye Uwanja wa Goodison Park juzi na kuweka historia ya kuwa bao la nne la haraka zaidi kwenye ligi hiyo.**



"Unajua katika maisha ya soka utapata kupanda na kushuka, sikutaka kupoteza kazi yangu. Lakini wakati huo huo naangalia nyuma sasa na labda ni jambo bora zaidi lililonipata," **Kocha wa zamani wa Brighton, Graham Potter, ambaye kwa sasa anainoa West Ham, akieleza kutojutia kutimuliwa na Chelsea mnamo Aprili 2023, chini ya miezi saba baada ya kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel aliyetimuliwa hapo Stamford Bridge Septemba 2022. Potter alitoa kauli hiyo jana kuelekea mchezo wao wa leo dhidi ya Chelsea.**



Nipashe Spotika

NIPASHE JUMATATU FEBRUARI 3, 2025

# USIYOYAJUA TIMU KUNDI MOJA NA TAIFA STARS AFCON 2025

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA imepangwa kwenye Kundi C, katika droo ya fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025, iliyochezeshwa hivi majuzi nchini Morocco. Iko na timu za Nigeria, Uganda na Tunisia.

Baada ya upangwaji, kumezuka mijadala mikali kutoka kwa baadhi ya wadau na mashabiki wa soka juu ya ugumu wa kundi ambalo Taifa Stars imepangwa.

Wengi hawasemi kuwa si kundi la kifo, ila ni kundi gumu ambalo Stars inatakiwa kufanya kazi ya ziada ili kusonga mbele.

Sababu kubwa ni timu ambazo imepangwa nazo. Nigeria ni moja kati ya majina makubwa si barani Afrika tu, bali duniani pale linapokuja suala la mpira wa miguu.

Tunisia nayo ni hivyo hivyo, ni moja kati ya timu kubwa ya kutisha linapokuwa suala la soka barani Afrika na hata duniani.

Uganda si timu ngumu au yenye jina sana kwenye soka barani Afrika, lakini ni moja kati ya timu inayoipa ugumu na changamoto kubwa Tanzania linapokuja suala la soka, iwe timu za wakubwa, wanawake mpaka vijana wa umri wote.

Katika makala haya tumekusanya historia, rekodi na takwimu za timu zilizo kwenye Kundi la Stars na kukuletea mengi juu ya timu hizo, twende sasa...



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Nigeria, 'The Super Eagles', wakishangilia kufuzu fainali za AFCON zitakazofanyika mwaka huu nchini Morocco. Ndiyo timu iliyotwaa ubingwa huo mara nyingi zaidi kwenye Kundi C, ambalo lina Tanzania, Tunisia na Uganda. **PICHA: MTANDAO**

### 1# Nigeria ( The Super Eagles)

Ni moja kati ya timu za kuogopwa, si barani Afrika, bali hata inapofuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia.

Hii ni moja ya timu ambazo zikiingia kwenye hatua hii, lengo si kufuzu kwenye kundi, bali kutwaa ubingwa wenyewe.

Ndiyo timu iliyochukuwa ubingwa wa AFCON mara nyingi kwenye kundi hilo. Imelitwaa mara tatu, 1980, 1994, na 2013. Mara ya kwanza ilikuwa ni 1980, ilipotwaa kwa kuifunga Algeria mabao 3-0, mechi iliyochezwa, Machi 22, Uwanja wa Surulere, nchini Nigeria ambapo michuano hiyo ilifanyika.

Taifa Stars ilishiriki michuano hiyo kwa mara ya kwanza, baada ya kufuzu 1979, na awali ilikuwa kundi moja na mabingwa hao, zikiwa Kundi A, pamoja na timu za Misri na Ivory Coast.

Ilitwaa tena mwaka 1994 kwenye fainali zilizofanyika nchini Tunisia, ambapo iliichapa Zambia 2-1 katika mchezo wa fainali uliochezwa, Uwanja wa El Menzah, Aprili 10, mabao yakifungwa na Emmanuel Amunike la Zambia likifungwa na Elija Litana. Ikumbukwe Zambia ilikuwa na kikosi kipya, baada ya kile cha kwanza kufariki kwenye ajali ndege iliyotokea mwaka mmoja nyuma, Aprili 27, 1993 nchini Gabon.

Mara ya tatu na mwisho, iliuchukua nchini Afrika Kusini, ilipoifunga Burkina Faso kwenye mchezo wa fainali, uliopigwa, Uwanja wa FNB, Johannesburg.

Timu ya Taifa ya Nigeria, imefanikiwa kuingia AFCON za 2025 kwa kuongoza Kundi D, ikimaliza na pointi 11.

### 2# Tunisia (The Eagles of Carthage)

Kama Nigeria, ni timu ambazo zinaanza AFCON zikiwa na nia moja tu ya kwenda kulibeba kombe, na haijalishi michuano hiyo inafanyika nje ya ardhi yao.

Tunisia ni moja kati ya timu tishio si kwenye kundi, bali kwa timu zote zinazoshiriki michuano hiyo.

Rekodi zinaonesha kuwa imelitwaa kombe hilo mara moja, 2004, kwenye fainali zilizopigwa nchini kwao.

Katika mchezo wa fainali uliochezwa, Februari 14, 2004 iliifunga Morocco mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Novemba 7 Stadium, jijini Tunis.

Imefanikiwa kutinga fainali za AFCON zinatazopigwa baadaye mwaka huu nchini Morocco, kwa kumaliza nafasi ya pili Kundi A, ikiwa na pointi 10, lililoongozwa na Comoro iliyomaliza na pointi 12.

### 3# Uganda (The Cranes)


Uganda ni timu yenye mzani kama Tanzania, ikiwa ni timu ambayo haijafanya maajabu yoyote kwenye michuano hiyo tangu ianzishwe 1957.

Si tu kwamba haijawahi kutwaa ubingwa, lakini kama ilivyo Stars, mafanikio yao makubwa mara nyingi ni kuvuka tu hatua ya makundi.

Hata hivyo, kwa mujibu wa rekodi, inaipa sana changamoto Tanzania kila zinapokutana kwenye michuano yoyote ile, iwe AFCON, au CECAFA na kuwa kama watani wa jadi hivi, kwani zikikutana huwa 'panachimbika.'

Uganda imefuzu kutoka Kundi K, ikimaliza nafasi ya pili nyuma ya Afrika Kusini. Wakati Sauzi hao wakimaliza na pointi 14, Uganda ilihitimisha na alama 13.

### JE, WAJUA?



BAO alililofunga Abdoulaye Doucoure katika sekunde ya 10, wakati Everton ikishinda 4-0 dhidi ya Leicester City kwenye Uwanja wa Goodison Park juzi, linashika nafasi ya nne kwa kuwa la mapema zaidi kuwahi kufungwa katika historia ya Ligi Kuu ya England. Bao hilo lilikuwa la haraka zaidi kuwahi kufungwa na mchezaji wa Everton na ni Shane Long, Philip Billing na Ledley King pekee ndio waliofunga kwa haraka zaidi kwenye ligi hiyo.

# Wanaotoa elimu usalama barabarani kimaslahi waonywa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imezionya taasisi zisizo za kiserikali zinazotoa elimu ya usalama barabarani kuacha kujipatia fedha kinyume na sheria.

Onyo hilo limetolewa juzi na Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Ardhini, Ezekiel Emmanuel alipokuwa akizungumza na mabalozi wa usalama barabarani Mkoa wa Dodoma.

Alisema bado kuna changamoto kwa baadhi ya taasisi zinazotoa elimu ya usalama barabarani kutoa elimu hiyo kwa malengo yao binafsi ili waweze kujipatia fedha kwa njia ya rushwa badala ya malengo halisi.

Alisema miongoni mwa taasisi hizo baadhi yao wamethubutu kutumia majina ya taasisi mbalimbali kama vile Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, TANROADS na TARURA ili waweze kuaminiwa wakati siyo kweli.

"Zimekuwa zikijinadi kwa kujitambulisha kuwa wanafanya kazi kwa kushirikiana na taasisi hizo,wakati siyo kweli na wanafanya hivyo ili waweze kujipatia fedha kutoka kwa wadau na jamii.

"Wengi wamekuwa wakitumia majina ya taasisi hizo za kiserikali ikiwemo LATRA kwa kizingizio cha kuelimisha jamii elimu ya usalama barabarani wakati hakuna mkataba wowote unaoonyesha makubaliano hayo," alisema.

Akizungumza na mabalozi wa usalama wa barabarani (RSA), aliwaomba kutumia nafasi yao kutoa elimu sahihi kwa jamii inayowazunguka ili wawe na ufahamu wa usalama wao.

Alisema wakifanya hivyo watasaidia jamii katika kutambua haki zao wanazotakiwa kizipata kupitia kwenye vyombo vya usafiri na hata kwenye matumizi ya barabara.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Mabalozi wa Usalama Barabarani Mkoa wa Dodoma, John Luganga, akizungumza kwenye ziara hiyo aliwaomba wadau wanaojihusisha na utoaji wa elimu kufanya kazi hiyo kwa uaminifu ili kuaminiwa na watoa maamuzi.

Kadhalika aliiomba serikali kuwachukulia hatua za kisheria wanaotoa elimu ya masula ya usalama barabarani ambao siyo waaminifu kwa kuwa wanaharibu maadili ya utendaji wa kazi.

# Watumishi waliotafuna mil. 550/- wapewa siku 30 kuzirejesha

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATUMISHI na mawakala halmashauri za wilaya za Mkoa wa Singida wamepewa mwezi mmoja kurejesha zaidi ya Sh. milioni 550 walizofuja, ambazo walizikusanya kama ushuru wa mifugo kwenye minada zaidi ya miaka mitano iliyopita.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alitoa agizo hilo juzi baada ya timu ya maofisa kutoka Wizara ya Fedha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwasili mkoani hapa kwa ajili ya kufuatilia fedha ambazo zina miaka mitano zilitafunwa na watumishi hao.

"Walipewa dhamana ya kukusanya pesa za serikali na kuzipeleka benki lakini wanakaa nazo mfukoni na tunaona kama hela hizi ni za kwetu. Hili haliwezekani ifikapo mwishoni mwa Februari fedha zote ziwe zimerejeshwa na baada ya hapo hatua za kinidhamu zichukuliwe na nipewe taarifa," alisema.

Ofisa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Gibonce Kayuni, alisema fedha hizo zilikusanywa na watumishi na mawakala hao kuanzia mwaka 2019 hadi 2024, walitakiwa kuzipeleka benki ziingie kwenye mfuko mkuu wa serikali lakini hawakufanya hivyo hadi sasa.

"Fedha hizi zinatokana na ushuru wa mifugo kwenye minada ambazo ng'ombe mmoja anatozwa Sh.7,500 na kati ya hizo Sh.5,000 huwa zinabaki halmashauri kwa ajili ya kuhudumia minada na Sh.2500 zinakwenda kwenye mfuko mkuu wa serikali kwa ajili ya kutumika kwenye shughuli za maendeleo nchini," alisema.

**"Walipewa dhamana ya kukusanya pesa za serikali na kuzipeleka benki lakini wanakaa nazo mfukoni na tunaona kama hela hizi ni za kwetu. Hili haliwezekani ifikapo mwishoni mwa Februari..."**

Kayuni alisema watumishi lazima watambue kuwa wanapopewa jukumu la kukusanya fedha za serikali wanapaswa kuifanya kazi hiyo kwa uaminifu.

Ofisa Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Abdul Danchi, alisema kiasi kilicholipwa kwa Mkoa wa Singida ni asilimia 12 tu ambapo jumla ya deni lote lilikuwa ni Sh.milioni 622.6 lakini zimelipwa kidogo na kubakia Sh.milioni 550.

Danchi alisema kitendo cha kukaa na fedha za serikali ni kuinyima serikali nguvu ya kutekeleza majukumu yakiwamo kulipa mishahara na shughuli za maendeleo ya kijamii.



Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Eva Kiaki Nkya (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kurugenzi ya Usimamizi wa Mashauri, Hawa Mnguruta (wa pili kushoto), kuhusu mifumo mbalimbali ya TEHAMA iliyopo ndani ya Mahakama, alipotembelea maonesho ya Wiki ya Sheria iliyohitimishwa katika viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Bil.3/- zatengwa ununuzi vifaa shule 20

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), katika mwaka huu wa fedha imetenga Sh. bilioni tatu kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na uboreshaji wa miundombinu katika shule 20 nchini.

Shule hizo ni zile zinazotoa mafunzo ya amali kwenye fani za kilimo, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), mapishi, ushonaji, michezo na sanaa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki mkoani Dodoma na Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dk. Erasmus Kipesha, kwenye maonesho ya uzinduzi wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la 2023, jijini Dodoma.

Alisema (TEA) imejipanga kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia mafunzo ya amali kama sehemu ya kuunga mkono utekelezaji wa Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Alisema jukumu la TEA ni kusimamia uboreshaji wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia, huku akisisitiza kuwa utekelezaji wa sera mpya ya elimu unahitaji miundombinu imara na vifaa vya kutosha kwa ajili ya mafunzo ya amali.

Dk. Kipesha alisema kuwa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haiwezi kutekelezwa kwa ufanisi bila kuboresha miundombinu, hivyo TEA ina jukumu kubwa la kuhakikisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia yanaboreshwa kwa viwango vinavyohitajika.

Alisema katika kutekeleza Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, TEA itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu kutafuta rasilimali fedha ili kuhakikisha miundombinu ya mafunzo ya amali inaboreshwa na vifaa vinapatikana kote nchini.

Alisema TEA kupitia mfuko wa elimu imekuwa ikisaidia uboreshaji wa miundombinu kuwezesha wanafunzi kusomea kwenye mazingira mazuri hali ambayo imekuwa ikisaidia kwa kiwango kikubwa kuongeza ufaulu wao.

Alisema hivi karibuni wanafunzi 400 wa kike kutoka mikoa ya Pwani na Lindi walipata huduma ya mabweni kupitia ufadhili wa TEA ambayo ilifadhili ujenzi wa mabweni matano katika shule tatu za mikoa hiyo.

Alisema Shule ya Sekondari Kwala iliyoko Chalinze Mkoa wa Pwani ilijengewa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 160 kwa gharama ya Sh. milioni 228.

Pia alisema kupitia mfumo wa elimu wa taifa TEA ilifanikiwa kukamilisha ujenzi wa nyumba sita za walimu wa Shule ya Vikumburu wilayani Kisarawe Mkoa wa Pwani zilizogharimu Sh. milioni 185.

Alisema kukamilika kwa nyumba hizo kumesababisha walimu sita na familia zao wamehamia kwenye nyumba hizo zilizoko maeneo ya karibu na shule hali ambayo inawapa fursa nzuri ya kujiandaa kufundisha.

Alisema mfuko wa elimu wa taifa umekuwa ukipokea rasilimali fedha na vifaa ambavyo hukusanywa na kuratibiwa na TEA na kufadhili miradi mbalimbali ya elimu nchini kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi.

Alisema TEA imepewa jukumu la kuhamasisha wadau mbalimbali nchini na nje ya nchi kuchangia rasilimali fedha na vifaa kusaidia juhudi za serikali kuinua ubora wa elimu na kuongeza upatikanaji wa elimu kwa usawa.





# Wasiojulikana waiba nyaya, kuharibu transfoma 36

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

WATU wasiojulikana wameanza kuhujumu miundombinu ya umeme katika jiji la Mbeya kwa kuiba baadhi ya vifaa, hali ambayo inasababisha wananchi kukosa huduma hiyo na kulisababishia hasara Shirika la Umeme nchini (TANESCO).

Akitoa taarifa ya hujuma hizo, Ofisa Uhusiano wa TANESCO Mkoa wa Mbeya, Christina Shoki alisema katika kipindi cha miezi mitatu transfoma 36 za umeme zimeharibiwa pamoja na wizi wa nyaya na vifaa vingine muhimu.

Alisema hali hiyo imekuwa ikilisababishia hasara shirika hasa kwenye urejeshaji wa miundombinu hiyo, huku akidai kuwa baadhi ya vifaa hivyo vikiibwa vinasababisha trasfoma hizo kuungua na kusababisha huduma kukosekana kwa wananchi.

Alisema hujuma iliyofanyika katika kipindi cha miezi mitatu ni kubwa zaidi kuwahi kutokea na hivyo akawaomba madiwani wa Jiji hilo kushirikiana na shirika hilo kukabiliana na wahujumu hao ili kuliokoa shirika na kuhakikisha wananchi wanapata huduma wanayostahili.

Alisema transfoma nyingi ziko kwenye maeneo ya makazi ya wananchi hivyo kuna uwezekano wananchi hao wanawajua watu wanaofanya hujuma hizo.

"Tunawaomba sana madiwani ninyi ni wadau muhimu sana, tusaidiane kuimarisha ulinzi kwenye maeneo ya miundombinu hii, hujuma hizi zinatusababishia sisi sote tukose huduma, lakini pia ni hatari kwa sababu transfoma hizi ziko kwenye makazi ya watu," alisema Shoki.

**"Tunawaomba sana madiwani ninyi ni wadau muhimu sana, tusaidiane kuimarisha ulinzi kwenye maeneo ya miundombinu hii, hujuma hizi zinatusababishia sisi ..."**

Alisema wahujumu hao wanaiba nyaya za shaba ambazo zipo ndani ya transfoma hizo ambazo ndizo zinalinda mashine hizo zisife na kwamba baada ya kuhujumiwa ndani ya muda mfupi zinaungua na kusababisha huduma kukosekana kwa wananchi.

Diwani wa Kata ya Iganzo, Daniel Mwanjoka aliwaomba maofisa wa TANESCO kuandaa utaratibu wa kufanya mikutano na wananchi katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kutoa elimu ili kuzuia matukio hayo yasiendelee.

Alisema baadhi ya taasisi zimekuwa zikiwaomba madiwani na wenyeviti wa serikali za mitaa kuwaalika kwenye mikutao yao ya hadhara ili waitumie kutoa elimu kwa wananchi.

Alisema taasisi kama Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU) zimekuwa zikitumia utaratibu huo kufikisha elimu kwa wananchi.

Mstahiki Meya wa Jiji la Mbeya, DorMohamed Issa aliwataka wananchi wanaofanya hujuma hizo kuacha kwa maelezo kuwa watakapokamatwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ambazo zitawaumiza.

Aliwataka madiwani kushirikiana na TANESCO kutoa elimu kwa wananchi kwenye maeneo yao ili washiriki kwenye ulinzi wa miundombinu hiyo na umuhimu wa huduma hiyo kwao.

Alisema yeyote atakayekamatwa akifanya hujuma hizo anatakiwa kuchukuliwa hatua ili iwe fundisho kwa wananchi wengine ambao wanapanga kufanya vitendo hivyo haramu.



Watendaji wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpiga Kura mkoa wa Tanga, wakila kiapo cha kujitoa uanachama wa vyama vya siasa na kile cha kutunza siri kabla ya kuanza kwa mafunzo ya siku mbili kwa watendaji hao, jijini Tanga jana. Viapo hivyo ni maandalizi ya zoezi la uboreshaji wa daftari hilo kwa mikoa ya Tanga na Pwani kuanzia Februari 13 hadi 19 mwaka huu, ambapo vituo vitakuwa vinafunguliwa saa 02:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni. **PICHA: INEC**

## Wakazi Nyanda za Juu Kusini waitwa kupima saratani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, imewataka wananchi mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kujitokeza mapema kupata huduma za uchunguzi wa aina mbalimbali za saratani.

Daktari Bingwa wa saratani katika Hospitali hiyo, Dk. Mathias Banzi aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Saratani Duniani ambayo hufanyika Februali 4 kila mwaka.

Alisema saratani ni miongoni mwa magonjwa hatari kwa maisha ya binadamu ambapo alisema saratani inaathiri wananchi wa rika zote na jinsi zote na hivyo akawataka wananchi kujitokeza kupima ili wawahi matibabu.

Alisema saratani ina uwezo wa kumpata binadamu kwenye kiungo chochote chenye seli hai na kwamba tatizo hilo husababishwa na ongezeko lisilokuwa la kawaida la seli hai hizo.

Alisema kwa Tanzania aina ya saratani inayoongoza kuwashambulia wanawake ni saratani ya mlango wa kizazi ikifuatiwa na saratani ya matiti na kwamba saratani hizo zinasababisha vifo vingi.

"Kwa wanaume aina ya saratani inayoongoza ni tezi dume ikifuatiwa na saratani ya mfumo wa chakula, tunawaalika wananchi wote kujitokeza kuja kufanyiwa uchunguzi ambao utafanyika bila malipo yoyote," alisema Dk. Banzi

Alisema saratani yoyote inatibika kirahisi inapokuwa katika hatua za awali na hivyo akawataka wananchi kujitokeza kupima ili wakibainika kuwa na viashiria vya ugonjwa huo waanze matibabu.

# Taasisi za umma zapokea msaada vifaa vya mil.39/-

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

VIFAA vya Sh. milioni 39 vimetolewa kwenye taasisi za umma katika Tarafa ya Kipembawe Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya kwa ajili ya kuboresha mazingira ya taasisi hizo kwenye utoaji wa huduma kwa wananchi.

Vifaa hivyo ambavyo ni kompyuta, madawati, meza, viti na mifuko ya saruji, vimetolewa na kampuni ya ununuzi wa tumbaku ya Premium Active Tanzania ikiwa ni sehemu ya urejeshaji wa faida kwenye jamii.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Harry Klonaridis alisema vifaa hivyo ni kwa ajili ya kutumika kwenye taasisi za umma hasa shule za msingi na za sekondari pamoja na ofisi za vijiji.

Alisema waliamua kutoa vifaa hivyo kwenye taasisi zilizoko kwenye Tarafa ya Kipembawe kwa sababu ndiyo tarafa inayozalisha tumbaku katika wilaya hiyo na vyama vingi vya msingi vya wakulima vinawauzia zao hilo.

"Tunaamini vifaa hivi vitawafikia wananchi wengi zaidi hasa wakulima ambao tunafanya nao biashara, lengo letu ni kuona wananchi katika maeneo ambayo kampuni yetu inafanya kazi wanapata maendeleo," alisema Klonaridis.

Meneja wa Operesheni wa kampuni hiyo, Nicco Roussos alisema vifaa hivyo vimenunuliwa kwa kuzingatia mahitaji ya walengwa kama walivyoomba, hivyo anaamini vitasaidia kuleta tija katika maeneo hayo.

Alisema kila kijiji kimepatiwa vifaa hivyo kulingana na maombi yake kwa maelezo kuwa kuna baadhi waliomba meza za ofisini, wengine mashine za kudurufu na baadhi waliomba kuboreshewa mazingira ya shule.

Alisema mbali na vifaa hivyo pia wamechonga madirisha ya vioo ambayo yatapelekwa katika majengo ya shule na ofisi katika maeneo yenye uhitaji.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbarack Batenga aliishukuru kampuni hiyo kwa uamuzi huo wa kurejesha sehemu ya faida yake kwa wananchi na akazitaka kampuni zingine kuiga mfano huo.

Aliwataka wakulima wa eneo hilo kuongeza uzalishaji na kuhakikisha wanazalisha kwa viwango vinavyotakiwa huku akiwataka kuepuka kushiriki vitendo viovu hasa utoroshaji wa tumbaku.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Cuthbert Mwinuka ambaye pia ni Ofisa Kilimo wa Wilaya hiyo aliwataka wanufaika wa vifaa hivyo kuvitunza na kuvitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alisema baadhi ya vifaa hivyo ni vya kisasa na hivyo vinahitaji watumiaji kupata mafunzo maalumu ili wavitumie vizuri bila kuviharibu na hivyo akawataka watumiaji kwenda kujifunza namna sahihi ya kuvitumia.



# ZAWA yalaani wizi wa miundombinu ya maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Maji Zanzibar (ZAWA) imesikitishwa na tabia ya baadhi ya watu kuiba miundombinu ya maji na kusababisha usumbufu wa upatikanaji wa huduma ya maji katika baadhi ya maeneo.

Meneja wa mradi wa uimarishaji huduma za maji Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rashid Mohamed Yussuf, alisema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu uwepo wa taarifa za kuibiwa kwa miundombinu ya maji.

Alisema miongoni mwa maeneo yaliyofanyiwa hujuma hizo ni Mwera Mwembemchomeke, Bumbwisudi, Jambiani pamoja na kukatwa bomba maji zinazoelekea Nungwi kipindi cha nyuma.

Alisema wahujumu hao hukata na kuchukua waya za shaba kwenda kuuza kwa kupata pesa hali inayoongeza mzigo kwa serikali.

"Zinazofanywa ni hujuma. Wananchi wengi hukosa maji na serikali kupata hasara ya kununua vifaa kila baada ya muda," alisema.

Aidha alisema hujuma nyingine ni kuziba na kukata bomba za maji kwa makusudi ili wamiliki wa magari wanaohusika na biashara ya maji waendelee na shughuli zao.

Alisema bomba la maji linalotoka Tazara kuelekea Kijiji cha Nungwi lilikatwa na kueleza kuwa eneo hilo linafanyiwa hujuma za mara kwa mara hali inayosababisha wananchi wa Nungwi kukosa maji baadhi ya maeneo.

Sambamba na hayo alisema wanatarajia kuweka walinzi wa kudumu kwa maeneo yenye visima kupunguza changamoto hiyo ya kuibiwa miundombinu ya maji na kuwataka wananchi kuwa walinzi wa miundombinu.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo (kulia) akikabidhi funguo ya trekta kwa Katibu wa kikundi cha wanawake cha Malambo A, Khadija Ng'ombo lililotolewa na Halmashauri ya Nachingwea juzi, kutokana na mkopo wa asilimia 10. Takribani Sh. Milioni 811 zimetolewa mkopo kwa vikundi 60 vya wanawake, vijana na wenye ulemavu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mizani ya pamba yadaiwa kuwaingiza hasara wakulima

**Na Shaban Njia**

WAKULIMA wa pamba katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameilalamikia mizani inayotumika kupima zao hilo kuwa inawaingizia hasara.

Kadhalika, wameilalamika bodi ya pamba kwa kuchelewesha kuwapatia viwatilifu na bomba za kupulizia dawa shambani hali inayosababisha wadudu kushambulia mmea na kupata mavuno kidogo kulinganisha na ukubwa wa mashamba wanayoyalima.

Waliwasilisha malalamiko hayo juzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Aanamringi Macha wakati wa ziara yake ya kukagua hali ya uzalishaji wa zao hilo.

Mkulima wa Kijiji cha Manungu Kata ya Uyogo, Juma Athumani alisema wamekuwa wakipata hasara kila msimu kwasababu ya mizani wanayoitumia sokoni vijijini kutofautiana na ile ya viwandani.

Alisema hali hiyo inawakatisha tamaa ya kuendelea kuzalisha zao hilo kwa wingi kulinganisha na mazao mengine na kuiomba serikali kuingilia kati na kutatua tatizo hilo.

"Tunawalalamikia wahasibu wetu kila masoko tukijua wao ndiyo wanatuingiza hasara kumbe mizani yetu tunayotumia inatofautiana na ile ya viwandani hasa wakati wa kupima gari lililobeba pamba, tunaomba serikali iangalie namna ya kulitatua hili ili tusikate tamaa ya kulima zao hili," alisema Athumani.

Andrew Iboliti alisema viwatilifu na bomba zinazotumika kupulizia dawa shambani haziwafikii kwa wakati, wadudu kushambulia zao hilo na wakati mwingine wanalazimika kuazima kwa wakulima wenzao.

Mkaguzi wa pamba Wilaya ya Kahama, Emmanuel Kileo alikili kuwepo kwa malalamiko hayo na kusema kunapotokea shida ya kupishana kwa mizani wanasitisha ushushaji na kuanza kupima upya na kupata uwiano sawa na mizani yote.

Alisema bomba hizo ni gharama kubwa na zinapopatikana zinafikishwa katika vyama vyao vya msingi isipokuwa wale wenye hekari tano na kuendelea wanapewa moja kwa moja na msimu huu wamepokea bomba 1,500.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha aliigiza bodi ya tumbaku kuhakikisha inawafikia wakulima, kuwasikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili ili kuhakikisha uzalishaji wa zao hilo unaongezeka kwani ndiyo moja ya kazi aliyopewa na Rais Samia Suluhu Hassani.

Aidha, aliwataka maofisa kila kijiji na kata kuhakikisha wanawakumbusha wakulima kanuni 10 za kilimo hicho ikiwa ni pamoja na kuwashauri namna ya kulima kisasa ili kuondokana na kupata kila 700 katika hekari 10, huku akiwasisitiza wakulima kuacha kuuza pamba kinyemela.

# SJMT, SMZ kuimarisha uzalishaji, usalama wa chakula

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MRATIBU wa mradi wa kuendeleza mifumo ya chakula, matumizi na urejeshaji wa ardhi, Miza Suleiman Khamis, amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zitaendelea kuimarisha misitu katika maeneo yaliyoharibiwa, ili kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula.

Akiwasilisha andiko la mradi wa mfumo wa chakula na matumizi ya ardhi kwa wadau mbalimbali, alisema mradi huo utashughulika na maeneo yaliyokatwa miti, kilimo kisichofaa na kuweka mifumo bora ya maji na ardhi.

Miongoni mwa wadau walioshiriki mkutano huo ni maofisa kilimo, watendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI), Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Halmashauri za Mkoa wa Kaskazini Unguja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza katika kitengo cha Idara ya Mazingira.

Miza ambaye pia ni Ofisa Mkuu katika Idara ya Misitu, alisema lengo la mradi huo ni kukuza usimamizi jumuishi wa rasilimali ardhi, maji, urejeshaji wa mnyororo wa thamani wa zao la mpunga ili kuzuia ukataji wa miti na uharibifu wa ardhi.

Aidha alisema kuwa Wizara ya Kilimo inaendelea na hatua za utekelezaji wa mradi huo ikiwemo kukamilika kwa kikao cha kwanza cha kamati ya uendeshaji ambacho kilipokea na kupitisha mapendekezo ya mpango wa utekelezaji ikiwemo Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Hivyo alisema kukamilika kwa hatua hiyo kumetoa fursa ya kuanza kwa utekelezaji wa shughuli za mradi huo unaotarajiwa kusaidia maeneo yaliyoharibika yakiwemo ya hifadhi za misitu na maeneo ya kilimo cha mpunga.

Mmoja ya waandaji wa mradi huo, Saleh Kombo Khiar, alisema mradi huo umebeba dhana mpya ambao utaweza kuangalia mandhari nzima ya eneo ambao utajumuisha katika sekta tofauti.

Alizitaja badhi ya sekta hizo kuwa ni kilimo, misitu, umwagiliaji maji, mifugo na maji, hivyo wananchi watarajie mafanikio makubwa ya kuweza kuboresha maeneo yaliyoharibika.

Ofisa Uzalishaji kutoka Idara ya Umwagiliaji, Rukia Wahabi Mohamed, alisema mradi huo utakua na fursa nyingi kwa Wazanzibari kutokana na malengo yake ya kukuza matumizi bora ya ardhi na mnyororo wa thamani wa zao la mpunga.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**RAJABU JUMA HAMISI,** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha Chuo chenye namba ya usajili **1538** kilichotolewa na Chuo cha Dodoma Mwaka 2012, **Cheti cha Matokeo ya Taaluma** kilichotolewa na Chuo cha Dodoma Mwaka 2012. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/3286/2025**

## KUPOTEA KWA CHETI NA RESULT SLIP



**ROSE KIRIMIA MTUI a**natangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne pamoja na Result slip zenye index namba **S0220/0071** vilivyotolewa na **TABORA GIRLS SEC. SCHOOL mwaka 1987. Y**eyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIL/MOS/1731/2025.**

## KUPOTEA KWA TRANSCRIPT



**HAIDALI BAKARI ADAM** anatangaza kupotea kwa transcript chenye No. **IRDP/BDF/16/1117** Kilichotelewa na **CHUO CHA MIPANGO DODOMA** mwaka 2019, Cheti hiki kimepotea Jijini DODOMA. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/3473/2025**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**RICHARD JOSEPH KISIKI** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (PASSPORT) yenye namba **TAE 090353** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 20/2/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/13667/2025.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**EMMANUEL GEPULA MASSE** anatangaza kupotelewa na cheti Cha kidato Cha nne chenye index namba **P0442/0067** kilichotolewa na Buhangija Sekondari, mwaka 2007. Cheti Cha kidato Cha sita chenye index namba **S0313/0574** kilichotolewa na Ikizu Sekondari, mwaka 2009. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MAR/MUS/1034/2025.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**RAJABU JUMA HAMISI,** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne chenye index namba **S0924-0117** kilichotolewa na shule ya sekondari Ikungi Mwaka 2008, Cheti cha kidato cha Sita chenye index namba **S.2326-0510** kilichotolewa na shule ya sekondari Mangwanjuki Mwaka 2011. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/3288/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ISSA RASHID TAYARI**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki (Haojue) yenye namba za usajili **MC 604 CMM,** (Chassis no **1c6pck25k0084941,** Engine no **156fmi-5a*d2f69380*** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye.

**PHQ/MOR/MOR/9370/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOSEPH NESTORY KAHINDI**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 975 DBG – BAJAJ BOXER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**PHQ/DAR/TEM/10928/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MODESTER MHINA SWILLA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T812DKY** aina ya **Toyota HARRIER,** Chassis No. **ACU300056809,** Engine No. **2AZB220530.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DOD/DOD/3412/2025**

## KUPOTELEWA NA HATI YA KIWANJA

**JOHN WILLIAM ZENDA** wa Kinondoni Dar es salaam anatangaza kupotelewa na Hati yenye Namba **DSMT1010593,** kilichopo Wilaya ya Kinondoni, Boko, **Block C,** Plot namba **2146, Area 360.00 sq** meter reg. plan namba **91711.** Ambacho kiwanja kilichotajwa hapo juu kilisajiliwa mnamo tarehe 02/06/2021. Taarifa ya polisi imetolewa kwa kumbukumbu Na.

**MBD/RB/168/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MIKA CLETUS MTEI**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 937 CVW** aina ya **TOYOTA NOAH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**PHQ/MOR/KIL/1884/2025.**

---

**SCABU MOTORS TANZANIA LIMITED**

Dodoma Tanzania, District Dodoma CBD, Ward Miyuji, Postal Code 41113, Street Msalato "A" P. O.Box 3007 DODOMA.

**NOTICE**

**TO**
**VUMILIA ANATHE MAPHIE**
**P.O.BOX.............**
**DODOMA**

**RE: CALL FOR UNPAID UP SHARES**

**TAKE NOTICE** that, Scabu Motors Tanzania Limited, through shareholder's special resolution dated 10th October 2024, resolved, among other issues, that, the company should call for unpaid up shares so as to generate capital for further investment.

**TAKE FURTHER NOTICE** that, you are in possession of 30 unpaid up shares; therefore, you are required to pay for the shares within 14 days commencing from the date of publish; failure to do that, the Company shall proceed to forfeit shares without further notice.

**Be informed,**

SCABU MOTORS TANZANIA LIMITED
C. M. MAGANGA
(Executive Director)

SCABU MOTORS TANZANIA LIMITED
25 JAN 2025
P. O. Box 3007
MSALATO-DODOMA

---

FORM 58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**

**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1806 OF 2025**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GLORY ELVIS MROSO**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ELVIS ELILEKIA MROSO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 25 day of February, 2025.

Dated at DAR ES SALAAM this 30 day of January, 2025.

Senior Resident Magistrate

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 32194 YA MWAKA 2024.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU RAMESH MAGANLAL BAKRANI**
**NA**
**NISHIL RAMESH BAKRANIA..................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5 Mwezi, February 2025. Saa 10:00 Asubuhi. Siku ambayo Shauri hili limepangwa kusikilizwa Mbele ya Mhe. Jaji G.N. BARTHY.

Imesainiwa Dar es Salaam, leo tarehe 23 Mwezi wa December, 2024.

NAIBU MSAJILI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 1516 YA MWAKA 2025**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA ROMANI PAUL MVAMBA...................MAREHEMU**
**ABDALLAH ROMANI MVAMBA................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikikwa mnamo au kabla ya tarehe 27 Mwezi February Mwaka 2025.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 30 Mwezi Januari Mwaka 2025.

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TUNDURU**

**Kituo cha MLINGOTI Mkowa wa RUVUMA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 192/2024**

**Jina la Mdai FAIRDEAL CREDIT LTD**

**Jina la Mdaiwa GIDION WILLY KAHOGGO**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**

**(Kanuni ya 62 ya Kanuni za Uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**

**KWA GIDION WILLY KAHOGGO**

KWAMBA Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 17 Mwezi wa 01 Mwaka 2025 kueleza kwanini hukumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo terehe 13 Mwezi wa 01 Mwaka 2025.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MLINGOTI-TUNDURU

---

FOMU MIRATHI - 2

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 113/2025**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU DANIEL RONALD MANGONI WA.....**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA DAVIS STANLEY MANGONI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 mwezi 02 mwaka 2025 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetokewa leo tarehe 21 mwezi 01 mwaka 2025.

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MTWARA LILILOPO MTWARA**

**MAOMBI YA 19 YA MWAKA 2023**

**MOHAMED BAKARI MPUNGA.....................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**GODFREY TOMASI TOMASI..................MJIBU MAOMBI NA 1**
**TERESIA MANDARASI CHITARE.........MJIBU MAOMBI NA 2**
**EMMANUEL JIKA MANGAPI ...............MJIBU MAOMBI NA 3**

**KUITWA SHAURINI**

**EMMANUEL JIKA MANGAPI, POPOTE ULIPO, FAHAMU** kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 10, Februari, 2025 saa 02:30 asubuhi.

**UNAAMRIWA** kuhudhuria mbele ya Baraza lililopo katika jengo la zamani la Halmashauri ya Wilaya ya Masasi siku hiyo iliyotajwa hapo juu bila ya kukosa.

Hati ya madau Pamoja na vielelezo vingine vyote kuhusiana na shauri hili utavipata kwenye masjala ya Baraza.

**FAHAMU KWAMBA** kushindwa kuhudhuria Barazani siku hiyo shauri litapangiwa kutajwa masjala ya Baraza

**FAHAMU KWAMBA** kushindwa kuhudhuria Barazani siku hiyo shauri litapangiwa kutajwa na kuamuriwa dhidi yako.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 13, January, 2025

NGUKULIKE, N.O
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MTWARA.

---

**MAHAKAMA YA WILAYA YA SINGIDA**
**MKOA WA SINGIDA**

**HATI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI Na. 225/2025**

**OMBI LA SAMSON MTUANGA HANGO KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU MARIA LINGWI RINGI.**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote wa mirathi ya marehemu MARIA LINGWI RINGI wanaalikwa kuja mahakamani kuhudhuria kesi mnamo tarehe 4 mwezi 2 mwaka 2025, kabla mwombaji huyo hatateuliwa kuwa msimamiz wa mirathi hiyo.

Tarehe 9/1/2025

Hakimu mkazi
Mahakama ya Wilaya Singida

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 30479 OF 2024**

**(In the matter of the Estate of the late LEAH ANDULILE MWAKISU of Dodoma City, at Kikuyu)**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MOHAMED MDEMU AND GEORGE MWAKISU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 02, 2025

Dated at Dodoma this 20 Day of January, 2025.

REGISTRY OFFICER
RESIDENT MAGISTRATE

**RESIDENT MAGISTRATE**

Presented for filing this 3 day of December, 2024.

---

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA



Baadhi ya raia wa DRC wakijiandaa kujiandikisha ili waweze kusaidia jeshi la nchi hiyo kupambana dhidi ya M23. **PICHA: MTANDAO.**

# Wanajeshi wawili wa Tanzania wauawa DRC

## • Ndayishimiye atahadharisha vita kuvuka mpaka

**Na Maulid Mmbaga**

WANAJESHI wawili wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) wamefariki katika mapigano dhidi ya kundi la waasi la M23 na vikosi vya walinda amani wakishirikiana na Jeshi la Kongo yanayoendelea katika mji wa Goma mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Pia ilielezwa kuwa wengine wanne wamejeruhiwa na wanaendelea na matibabu mjini Goma, na kwamba wanajeshi hao ni miongoni mwa waliokuwa wakishiriki shughuli za ulinzi wa amani nchini DRC chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa (UN) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Nchini DRC katika mji wa Goma kumeendelea kushuhudiwa mapigano dhidi ya waasi wa M23 walioteka eneo hilo na wanajeshi wa Kongo, hali ambayo imesababisha machafuko ikiwemo vifo vya zaidi ya raia 100 huku zaidi ya milioni moja wakikimbia makazi yao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano wa JWTZ Kanali Gaudentius Ilonda, taratibu za kuisafirisha miili ya marehemu pamoja na majeruhi waliotokana na mapigano hayo zinaendelea kupitia sekretarieti ya SADC.

"Pia vikundi vyetu vilivyoko nchini DRC viko salama, imara na vinaendelea kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo ya uongozi wa SADC," alisema Kanali Ilonda.

Wakati huo huo, Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, alionya kwamba mzozo wa DRC unaweza kusambaa na kuwa vita vya kikanda, akitahadharisha kwamba mgogoro huo ukienea na kuingia nchini kwake hatokubaliana nao.

Ilielezwa kuwa wanajeshi wa Burundi wamekuwa wakisaidia Jeshi la Kongo kupambana na waasi wa M23 wanaodaiwa kuungwa mkono na Rwanda, ambao siku chache zilizopita waliuteka mji wa Goma huku wakiendelea kusonga mbele kuelekea kusini.

Rais, Ndayishimiye alionya kwamba iwapo Rwanda itaendeleza kile alichokiita ushindi wake, vita vinaweza kusambaa hadi Burundi, jambo ambalo alisema halikubaliki.

Wakati mvutano ukiwa tayari umetanda kati ya Burundi na Rwanda, Umoja wa Mataifa ulionya kwamba mapigano ya moja kwa moja yanaweza kuzua marudio ya vita vya kikanda yaliyokuwa mwishoni mwa miaka ya 1990.

Ilielezwa kuwa awali Burundi ilikata uhusiano na Rwanda mwaka jana, ikiishutumu kwa kuwahifadhi waasi walioshambulia eneo lake miaka miwili iliyopita.

**MISAADA IRUHUSIWE**

Wakati hayo yakiendelea Shirika la kutetea haki za kibinadamu la 'Human Rights Watch' lilisisitiza Jeshi la Rwanda na kundi la waasi la M23 kuhakikisha kwamba kuna njia za kusafirisha misaada ya kibinadamu hadi kwa wakazi wa mji wa Goma.

Watetezi hao wa haki za binadamu walisema mapigano yanayoendelea kushuhudiwa mjini Goma yanaharibu vituo vya afya na kutatiza misaada inayowafikia wanaohitaji huko Goma.

Licha ya Rwanda kukanusha madai ya kuhusika kwenye mzozo wa Mashariki mwa DRC, Jamii ya Umoja wa Mataifa iliripoti kuwepo kwa majeshi ya Rwanda ndani ya Goma yanayopigana pamoja na waasi wa M23.

**HALI ILIVYO**

Kwa mujibu wa BBC, wataalamu wa masuala ya kivita wanakadiria kuwa kati ya wanajeshi 3,000 hadi 4,000 wa Jeshi la Rwanda wako nchini DRC, ikielezwa kuwa picha za kijiografia na ushuhuda zilionesha.

Pia kwa mujibu wa wataalamu wa Umoja wa Mataifa (UN) M23 hupewa mafunzo ya miezi mitano katika kambi ya Chanzu, na inaelezwa kuwa maofisa wa Rwanda mara nyingi walikuwepo eneo hilo.

Ilielezwa kuwa wapiganaji waliokamatwa wa M23 walisema kuwa wao ni wanyarwanda wanaojulikana kama 'Friendly Force' (vikosi rafiki), huku ripoti ya wataalamu ya mwezi Desemba 2024 ikielezwa kuwa neno hilo lilitumiwa na wote.

Wataalamu wa UN walisema uamuzi wa M23 wa kuteka mji wenye madini wa Rubaya mwezi Mei 2024, ulichochewa na hitaji la kimkakati la kushikilia biashara yenye faida kubwa ya madini ya Coltan ambayo yanatumika kutengenezea betri za magari ya umeme na simu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mashirika ya kijamii, hatua ya M23 kuudhibiti mji huo inawazuia mamilioni ya watu kupata huduma muhimu. Huku wakisisitizwa kuhakikisha kwamba njia za kuingiza maji safi, chakula na dawa zinafunguliwa mara moja.

Pia wapiganaji hao wa M23 walishauriwa kuhakikisha kwamba raia wanaokimbia mapigano wakitafuta hifadhi wanakubaliwa kufanya hivyo.

Mkurugenzi wa Shirika la Human Rights Watch Lewis Mudge, anayesimamia Afrika ya kati alisema "Jeshi la Rwanda linahitaji kuangazia hali mbaya ya kibinadamu inayoshuhudiwa baada ya maelfu ya raia kupoteza makazi yao wakikimbia vita Goma kwa sasa'.

"Pande zote kwenye mzozo huu zinahitaji kuhakikisha kwamba raia wanapata chakula, na huduma za matibabu na kwamba wahudumu wa afya na wale wa dharura wana uwezo wa kutembea kwa uhuru kutoa usaidizi," alisisitiza Mudge.

**HATARI YA MAGONJWA**

Mkuu wa Wakala wa Afya barani Afrika alisema hali katika mji wa Goma nchini DRC imegeuka kuwa dharura ya afya ya umma, akionya kwamba mapigano hayo yanaweza kuchochea milipuko ya magonjwa makubwa.

Ilielezwa kuwa kutokana na machafuko yanayoendelea kushuhudiwa mashariki mwa DRC, imesababisha eneo hilo kuwa na milipuko ya magonjwa ya kuambukiza baada ya kukosekana kwa huduza za kiafya.

Ikumbukwe kuwa siku chache zilizopita M23 walichukua udhibiti wa sehemu kubwa ya mji mkuu wa Kivu Kaskazini Goma, jiji lenye watu milioni tatu, huku milioni moja kati yao wakiwa wameyakimbia makazi yao.

Jean Kaseya, mkuu wa Vituo vya Afrika vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (Africa CDC), alisema hali hiyo ni mbaya, na kwamba ukosefu wa usalama na uhamiaji mkubwa wa watu kulichochea kuenea kwa virusi vya mpox.

Alisema aina ya clade 1b ya mpox, ambayo ilirekodiwa katika nchi nyingi ulimwenguni katika miezi ya hivi karibuni, iliibuka kwa mara ya kwanza katika mkoa jirani wa Kivu Kusini mnamo 2023.

"Goma imekuwa kitovu cha maambukizi na kusambaza mpox katika nchi 21 za Afrika. Hili si suala la usalama pekee ni dharura ya afya ya umma," alisema katika barua aliyotuma kwa viongozi wa Afrika.

"Vita hivi lazima vikome. Ikiwa hatua madhubuti hazitachukuliwa, haitakuwa risasi pekee ambayo itaua maisha, itakuwa ni kuenea kwa milipuko ambayo itatoka katika eneo hili dhaifu na uchumi mbaya wa jamii katika bara letu," alisema.

Kadhalika alieleza kuwa kudumu kwa migogoro hiyo pia kulisababisha kuenea kwa surua, kipindupindu na milipuko mingine, ikigharimu maisha ya maelfu.

Ilielezwa kuwa mzozo wa mashariki mwa DRC unaongezeka kwa kasi katika eneo ambalo limeshuhudia miongo kadhaa ya migogoro inayohusisha makundi mengi yenye silaha, ambayo katika miongo mitatu iliyopita yamegharimu maisha ya takriban watu milioni sita.

Wakati huo huo, waangalizi wa kimataifa walitoa tahadhari juu ya athari za kibinadamu za mzozo unaozidi kuongezeka katika mji wa Goma mashariki mwa DRC.

*CHANZO: MTANDAO*

# MAFUNZO FC YATEGEMEA WAPYA KUIMALIZA KVZ LEO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

HUKU ikitarajia kutoa nafasi kwa nyota wake wapya waliowasajili kipindi cha dirisha dogo la Januari, timu ya Mafunzo FC imepania kuibuka na ushindi katika mchezo wao leo, Jumatatu dhidi ya KVZ FC katika mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya PBZ.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Abdallah Bakari 'Edo', alisema katika mchezo wao wa mzunguko wa kwanza, timu hizo ziligawana alama kwa kutoka sare ya bao 1-1, hivyo hayatamani matokeo hayo kwenye mzunguko huu wa pili.

Alisema timu yake imefanya maandalizi mazuri ikiwamo kucheza michezo ya kirafiki na timu za ndani na nje ya Zanzibar dhidi ya Azam FC.

Edo alisema kupitia michezo hiyo ya kirafiki wameweza kuona ubora wa wachezaji wao pamoja na mapungufu ambayo wameyafanyia kazi katika uwanja wa mazoezi.

Alisema kupitia mchezo huo katika kuhakikisha hawapotezi lengo wamepanga kuwajumuisha wachezaji watatu wapya ambao wamewasajili kipindi cha dirisha dogo, Januari.

Alisema anaamini ingizo jipya hilo litaweza kuamsha zaidi ari ya wachezaji wao na kufanikiwa kuondoka na alama tatu.


"Muhimu ni kupata alama tatu, ndizo tunazozihitaji, na tumejipanga kuona tunakuwa ndani ya malengo yetu, wachezaji wana ari kubwa ya kufanya hivyo," alisema.

Aidha, akiwazungumzia wapinzani wao, KVZ FC, alisema ni miongoni mwa timu ambazo zinawachezaji wengi wazuri na vijana.

Alisema wanapaswa kuwa makini na kutojiamini kupita kiasi uwanjani ili wapinzani wao wasitumie mwanya huo kuwatibulia mipango yao.

Mafunzo FC na KVZ FC ni miongoni mwa timu ambazo zipo katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

**KAZI KAZI...**




Beki wa Yanga, Israel Mwenda, akicheza mpira kwa kichwa dhidi ya Beki wa Kagera Sugar, Abubakar Sabian, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda mabao 4-0. **MPIGAPICHA WETU**

# New City FC na matumaini kibao Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya New City FC kujikuta ikianza vibaya mchezo wao wa kwanza wa mzunguko huu wa lala salama kwa kupokea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Wanajeshi wa Kipanga FC, imesema bado ina matumaini ya kufanya vizuri michezo yao 14 iliyosalia na kufikia malengo yao.

Mchezo huo ni wa mzunguko wa 16 katika Ligi Kuu Zanzibar ambao ulichezwa juzi, Jumamosi katika Uwanja wa Cairo, Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha msaidizi wa New City FC, Razak Rajab, alisema kupoteza mchezo huo kumezidi kuwapa nguvu zaidi ili kuhakikisha michezo 14 iliyobaki wanaweze kufanikiwa kupigania kutoshuka daraja.

Alisema ingawa bado wanamichezo 14, lakini ushindi wa michezo ya mwanzo ndio ungewapa mwanga zaidi katika kutimiza mpango wao.

Rajab alisema bado wanakazi kubwa na ya yaziada katika kuhakikisha wanafanikiwa kushinda michezo iliyobakia ili kujilinda na kushuka daraja.

Aidha, akizungumzia mchezo huo walipoteza, alisema timu yake ilicheza vizuri, lakini ilishindwa kutambua mbinu za wapinzani wao wakati wa mchezo.

Alisema hawakuwa makini kipindi ambapo wapinzani wao wanamiliki mipira, lakini hata kuhakikisha wanalinda lango lao muda wowote.

"Tumepoteza mchezo muhimu hasa katika harakati zetu za kuhakikisha tunapata alama tatu ili kuinusuru timu kushuka daraja, hatupo nafasi nzuri katika msimamo wa ligi, inatubidi tupambane ili tufanikiwe," alisema.

Hata hivyo, alisema kupitia mchezo huo ataenda kuyafanyia kazi mapungu kadhaa ambayo ameyaona hasa umakini na kuongeza utimamu wa kimwili kwa viuingo wake.

Kwingeneko kwenye ligi hiyo, katika Uwanja wa Finya kisiwani Pemba, timu ya Mwenge nayo ilifanikiwa kuwaadhinu wapinzani wao, Tekeleza FC kwa bao 1-0.

## KMC FC kuanza kukarabati uwanja

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Klabu ya KMC, umesema upo katika hatua za mwisho kuanza maboresho ya uwanja huo baada ya kupokea barua kutoka Bodi ya Ligi, ikitaka baadhi ya maeneo yamaliziwe.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, jana, Meneja wa uwanja huo uliopo Mwenge, Dar es Salaam, Daniel Madenyeka, alikiri kupokea barua kutoka Bodi ya Ligi, akisema wanaifanya kazi, licha ya kwamba kabla ya hapo, tayari walikuwa na mpango huo.

"Nadhani Bodi ya Ligi wameona aidha tunachelewa, kwa hiyo wakaona watukumbushe kumalizia yale maeneo ambayo mchezo wa miguu unaweza kufanyika katika mazingira ambayo wachezaji, viongozi, waamuzi, wanakuwa na amani.

"Kabla ya kupata barua, Manispaa ya Kinondoni ilikuwa inaendelea na utaratibu wa kupata makandarasi wa kuendelea na ujenzi wa uwanja pale ulipoishia, kwa bahati nzuri ameshapatikana, hivi sasa ni taratibu za kiofisi zinamaliziwa kabla ya kuanza maboresho," alisema Meneja huyo.

## Wazawa Ikungi wasajili taasisi kuinua soka lao

**Na Jumbe Ismailly, IKUNGI**

JUMUIYA ya watu wanaoishi nje ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, wamesajili taasisi ya kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo kwa vijana kwa ajira endelevu ijulikanayo kama Ikungi Singida Sports Promosion (ISSP), itakayohakikisha michezo ndani ya halmashauri hiyo inanyanyuka sambamba na vijana kupata ajira kupitia sekta hiyo.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Ikungi Singida Sports Promosion, Salvatory Alute, aliyasema hayo kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi wakati wa hafla ya kuitambulisha taasisi hiyo na kukabidhi msaada wa mipira kwa baadhi ya shule za msingi na sekondari zilizopo katika halmashauri hiyo.

Alisema kwamba lengo la kuanzishwa kwa taasisi hiyo ni kuhakikisha michezo katika halmashauri hiyo, Mkoa wa Singida na baadaye katika nchi nzima inanyanyuka na vijana wanapata ajira na kurudisha nyumbani kile wanachokipata, hivyo kuchangia uchumi kukua katika eneo hilo huku wazazi na jamii kwa ujumla zikifaidika.

Aidha, Alute aliweka bayana kuwa kwa sasa wamebaini kwamba kuna baadhi ya watoto wenye vipaji vya michezo, lakini wanaishia kwenye ngazi za chini hivyo kutoonekana kwa sababu hakuna mtu wa kuwasaidia.

## ZISIKUPITE

### TOURE ATAKIWA MAN UNITED
MANCHESTER United imeongeza kasi ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Mali, El Bilal Toure mwenye umri wa miaka 23, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Stuttgart kutoka Atalanta. ***(TeamTalks)***

### DISASI NAYE AWINDWA
KLABU ya Tottenham Hotspurs imeonesha nia ya kumnunua mlinzi wa Chelsea, Axel Disasi mwenye umri wa miaka 26, iwapo uhamisho wa mlinzi wa England, Fikayo Tomori mwenye miaka 27, kutoka AC Milan utashindikana. ***(Telegraph)***

### NKUNKU BADO BAYERN
UHAMISHO wa Bayern Munich kwa mshambuliaji wa Chelsea, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 27, hautafanyika katika dirisha hili la usajili, lakini unaweza kufufuliwa msimu wa majira ya joto. ***(Christian Falk)***

### SYLLA AWANIWA SOUTHAMPTON
KLABU ya Southampton ina nia ya kutaka kumsajili beki wa Ivory Coast, Loubadhe Abakar Sylla mwenye umri wa miaka 22, kwa mkopo kutoka Strasbourg. ***(Fabrizio Romano)***

### CHILWELL KWA MKOPO
CRYSTAL Palace imewasiliana na Chelsea kuhusu kumsajili kwa mkpo beki wa England, Ben Chilwell, 28. ***(Athletic)***

### MALACIA KUONDOKA UNITED
PENDEKEZO la beki wa Manchester United, Tyrell Malacia kuhamishwa kwa mkopo kwenda Benfica limeshindikana, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, bado anaweza kuondoka Old Trafford. ***(Fabrizio Romano)***

### EDWARDS ATAKIWA BURNLEY
KLABU ya Burnley inakaribia kumsajili winga wa England, Marcus Edwards mwenye umri wa miaka 26 kutoka Sporting. ***(Sportsport)***

### KELLY KUHAMIA NEWCASTLE
MLINZI wa Newcastle United, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 26, anakaribia kuhamia Juventus inayoshiriki Serie A. ***(Chronicles)***

### GIMENEZ AKARIBIA MILAN
AC Milan inakaribia kumsajili mshambuliaji wa Feyenoord na Mexico, Santiago Gimenez mwenye umri wa miaka 23. ***(Goal)***

### KROUPI AWANIWA WEST HAM
KLABU ya West Ham imetoa ofa yenye thamani ya hadi pauni milioni 30 kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 18, Eli Junior Kroupi, ambaye kwa sasa yuko na Lorient. ***(Football Insider)***

### ILING-JUNIOR NA MIDDLESBROUGH
KLABU ya Middlesbrough ipo kwenye kwenye mazungumzo ya kumsajili winga wa Aston Villa, Samuel Iling-Junior mwenye umri wa miaka 21, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Bologna. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI ALIA NA RAFU MBAYA KWA MBAPPE

**Aliyemfanyia asema alijua haiwezekani kumzuia kwa kukimbia naye, hivyo alifanya...**

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti ametaja uamuzi wa kutomtoa kwa kadi nyekundu Carlos Romero wa Espanyol -ambaye baadaye alifunga bao pekee katika ushindi wa 1-0 wa timu yake dhidi ya Real Madrid - kuwa „hauwezi kueleweka", baada ya beki huyo kuomba msamaha kwa rafu yake dhidi ya Kylian Mbappe.

Romero alioneshwa kadi ya njano na mwamuzi Alejandro Muniz Ruiz kwa kumchezea vibaya Mbappe katika dakika ya 61, na kumwangusha fowadi huyo wa Madrid kwa kumkwatua kwa nyuma wakati alipokuwa anaelekea kufunga.

Beki huyo baadaye alifunga bao la ushindi dakika ya 85, huku kichapo hicho kikiwaacha vinara Real wakioongoza kwa pointi moja kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania dhidi ya wapinzani wao, Atletico Madrid.

"Uamuzi ambao mwamuzi na VAR aliuchukua hauelezeki," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi hiyo.

"Kila mtu aliona. Jambo muhimu zaidi ni kumlinda mchezaji. Ni faulo ya wazi. Faulo mbaya sana. Kwa bahati nzuri hakuna kilichotokea kwa upande wa kuumia, lakini VAR ipo kwa hilo. Haielezeki kwetu kwamba haikufanya hivyo."

Akizungumza baada ya filimbi ya mwisho, Romero alisema ameomba msamaha kwa Mbappe.

"Nilijua kuwa haiwezekani kumzuia Mbappe kwa kukimbia," alisema akiiambia DAZN.

"Nilifanya nilichoweza kumzuia. Changamoto ilikuwa mbaya kidogo, sikuipenda, na nikamwambia samahani."

Kocha wa Espanyol, Manolo Gonzalez, alisema hakukuwa na nia yoyote kwa Romero kumjeruhi Mbappe.

"Ilikuwa changamoto ngumu, lakini ilikusudiwa kusimamisha shambulio hilo, si kumuumiza mpinzani," alisema Gonzalez akiiambia DAZN.

Madrid pia walikasirishwa na uamuzi wa kipindi cha kwanza wa kukataa bao la Vinicius Junior kwa madhambi ya Mbappe.

"Mchezo ulikuwa mgumu," alikiri Ancelottii.

"Tulifanya mambo vizuri. Tulikuwa na udhibiti, zaidi ya yote katika kipindi cha pili, na tulipata nafasi. Tulikuwa na bao lililokataliwa.

"Tulikuwa na mashuti 20 kwenye lango. Espanyol walicheza vizuri katika mabadiliko, walilinda vema, walitukamata."

# Rashford kuamkia Aston Villa

**LONDON, England**

ASTON Villa wapo kwenye hatua ya mwisho kufikia makubaliano ya kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford, kwa mujibu wa ESPN.
ESPN iliripoti Ijumaa kwamba timu hiyo ya Kocha Unai Emery imeonesha nia ya kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa England, na sasa inaonekana kuna uwezekano Rashford kujiunga nao.
Rashford anatarajiwa kuhamia Villa Park na kukaa hadi mwishoni mwa msimu.
Villa wamekubali kugharamia sehemu kubwa ya mshahara wa Rashford, na bonasi zingine zinazohusiana na uchezaji wake.
Villa wamekuwa wakitafuta njia za kuimarisha safu yao ya ushambuliaji baada ya kukubali kumruhusu mshambuliaji Jhon Duran kwenda Al Nassr ya Saudi Arabia.
Pia kuna chaguo la kufanya uhamisho kuwa wa kudumu mwishoni mwa msimu.
Ikiwa Villa hawatachukua chaguo hilo, Rashford atatarajiwa kurejea Old Trafford majira ya joto.
Rashford mwenye umri wa miaka 27, anapatikana baada ya kutemwa na Kocha Mkuu wa United, Ruben Amorim.
Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba upendeleo wake ulikuwa kuhamia Barcelona.
Hata hivyo, matatizo ya kifedha ya timu hiyo ya LaLiga yalifanya makubaliano kuwa magumu.
Borussia Dortmund pia wameonesha nia ya kumtaka Rashford, lakini mshahara wake wa kila wiki wa pauni 350,000 kwa wiki ulionekana kuwa kikwazo kikubwa.

# Barca wamtafutia msaidizi Kounde

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA inafuatilia maendeleo ya beki wa kulia wa Monaco, Vanderson ili aweze kuwa msaidizi wa Jules Kounde upande wa beki wa kulia, kwa mujibu wa ripoti kutoka Hispania.
Miamba hao wa Katalunya wamekuwa wakihusishwa kwa kiasi kikubwa na mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford Januari, lakini inaonekana kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, atabakia Ligi Kuu England ambapo atajiunga na Aston Villa kwa mkopo.
Matatizo ya kifedha yanaendelea kuwasumbua Barcelona, ambao hawatarejea katika uwanja wao wa Spotify Camp Nou kwa wakati huku kukiwa na kucheleweshwa kwa kazi za ujenzi, lakini Mkurugenzi wa Michezo, Deco anaendelea kuwatafuta wachezaji wanaoweza kuimarisha kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Hansi Flick.
Jarida la Hispania la Mundo Deportivo linaripoti kwamba Vanderson wa Monaco ni mmoja wa wachezaji waliovutia macho ya kiungo huyo wa zamani wa Ureno, ingawa imeelezwa hapo awali kwamba Monaco hawataki kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.
Vanderson aliwasili Ufaransa Januari 2022, na kujiunga na Monaco kwa ada ya Euro milioni 11, na pamoja na kuichezea klabu hiyo zaidi ya mechi 100, amejitokeza kwenye ulingo wa Kimataifa wa Brazil.
Inaaminika thamani yake imeongezeka zaidi ya mara tatu tangu awasili Monaco, akisaidiwa na maonesho yake maarufu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.
Barcelona wanataka kumtafutia Jules Kounde msaidizi.
Nafasi ya asili ya Kounde ni kama beki wa kati, lakini alirudishwa tena na Xavi na sasa Flick kama beki wa kulia mwenye uwezo wa kuingia kwa kasi na kutoa usaidizi kwenye kufunga mabao.

# SALAH AMPIKU LAMPARD EPL




**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah amejivuta hadi nafasi ya sita kwenye orodha ya wafungaji mabao wa muda wote wa Ligi Kuu England (EPL), baada ya kufunga mawili wakati Liverpool ikishinda 2-0 dhidi ya Bournemouth Jumamosi.
Fowadi huyo wa Misri alianza kuiweka mbele timu hiyo ya kocha Arne Slot iliyopo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa mkwaju wa penalti dakika ya 30 kabla ya kumfunga golikipa Kepa Arrizabalaga zikiwa zimesalia dakika 15 kabla ya mchezo kumalizika katika Uwanja wa Vitality.
Bao la 177 na 178 la Salah kwenye Ligi Kuu lilimfanya kumpita gwiji wa Chelsea, Frank Lampard, wiki moja baada ya kumpita Thierry Henry aliyekuwa namba nane kwa bao lake dhidi ya Ipswich Town.
Bao lake la pili Jumamosi lilikuwa la 300 katika maisha yake ya soka. (Liverpool (235), AS Roma (34), Basel (20), Fiorentina (9) na Chelsea (2).
Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ana mabao matatu mbele ya Erling Haaland wa Manchester City na manne dhidi ya Alexander Isak wa Newcastle United katika mbio za kuwania kiatu cha dhahabu msimu huu.
Fowadi huyo pia amechangia pasi za mabao 13.
Salah ndiye mchezaji wa pili wa nje ya Ulaya aliyefunga mabao mengi zaidi katika historia ya mashindano hayo, nyuma ya Sergio Agüero (184).
Alan Shearer ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Ligi Kuu England akiwa amefunga mabao 260.
Salah yuko katika miezi sita ya mwisho ya mkataba wake pale Merseyside na yuko huru kufanya mazungumzo na klabu zilizo nje ya England kwa nia ya kusaini makubaliano ya awali ya mkataba ambayo yatamfanya ajiunge na timu mpya siku moja baada ya kumalizika kwa mkataba wake.
Wachezaji wenzake wa Liverpool, Virgil van Dijk na Trent Alexander-Arnold pia mikataba yao imebaki miezi sita.

# NBC YAJIPANGA KUIFANYA LIGI KUU BARA KUWA NAMBA MOJA AFRIKA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kwa mujibu wa Shirikisho la Kimataifa la Historia ya Soka na Takwimu (IFFHS), Ligi Kuu Bara kwa sasa ikishika nafasi ya nne kwa ubora barani Afrika, Wadhamini Wakuu wa ligi hiyo, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), wamesema licha ya mafanikio hayo makubwa yanayoendelea kushuhudiwa bado dhamira ya benki hiyo ni kuhakikisha ligi hiyo inashika nafasi ya kwanza kwa ubora barani Afrika.

Dhamira ya benki hiyo iliwekwa wazi mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Biashara wa benki hiyo, Joseph Lyuba, wakati wa hafla fupi ya kuhitimisha rasmi kampeni yake yenye falsafa ya kimichezo ya 'Shinda mechi zako Kinamna yako' ambapo ilikabidhi zawadi ya gari aina ya BMW X1 kwa Galus Peter Casto maruufu "Kweka", mfanyabiashara mdogo 'Machinga' kwenye Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam alieibuka mshindi.

Akizungumza kwenye hafla hiyo iliyofanyika kwenye tawi la benki hiyo Kariakoo, Lyuba alisema pamoja na kujivunia mafanikio ya ligi hiyo, benki hiyo ipo kwenye mkakati zaidi kuhakikisha kwamba inashirikiana na wadau zaidi ili kuongeza nguvu kwenye ligi hiyo lengo likiwa ni kuongeza hadhi ya ligi hiyo hadi kufikia nafasi ya kwanza barani Afrika.

"Mafanikio haya yanachochewa na ushirikiano mkubwa baina yetu kama wadhamini wakuu na wadau wenzetu wakiwamo Azam TV, wadau wote wa habari na mashabiki tukiongozwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF). Tunaamini mafanikio haya yatavutia wadau wengi zaidi na kwa pamoja tunakwenda kuifanya ligi hii kuwa namba moja barani Afrika," alisema.

Akizungumzia kampeni ya 'Shinda mechi zako Kinamna yako', Lyuba alisema ililenga kuchochea ukuaji wa uchumi miongoni mwa wateja wao kupitia uwekaji wa akiba.

"Tangu kuzinduliwa kwa kampeni hii inayotumia falsafa ya michezo kuboresha maisha ya wateja wetu Aprili mwaka jana, tumeweza kutoa zawadi za gari mbili aina BMW X1 kwa washindi wakuu pia tulitoa fursa kwa wateja hao kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo fedha taslimu, simu za mikononi, 'laptops', friji, 'tablets' za watoto, bima za afya pamoja na majiko ya kisasa ya kupikia," alisema.

Kwa mujibu wa Lyuba jumla ya zawadi zenye thamani ya Sh. milioni 200 zimetolewa kwa washindi mbalimbali wa kampeni hiyo tangu kuanzishwa kwake.

"Zaidi ya aina nane ya zawadi zilizotolewa kupitia kampeni hii zilikuwa zipo kimkakati zaidi tukilenga ziwasaidie wateja wetu kwenye kufanikisha majukumu yao kiuchumi ambayo ndio maana halisi ya 'Shinda mechi zako' zikiwamo nyenzo za biashara na vitendea kazi vitakavyoweza kuwarahisishia kazi zao," aliongeza.

Akifafanua zaidi kuhusu kampeni hiyo, Meneja Masoko wa Benki hiyo, Alina Kimaryo, alisema ilihusisha wateja wote waliokidhi vigezo na masharti na wanaohudumiwa na benki hiyo kupitia huduma zake mbalimbali zikiwamo akaunti za Chanua, Akaunti ya Malengo, Akaunti ya Mwalimu pamoja na akaunti ya Johari.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa zawadi yake, Kweka aliyeambatana na mke wake, Miriamu Kweka, pamoja na kuishukuru benki hiyo kwa makabidhiano hayo alisema ushindi huo umetokana na yeye kujiwekea akiba kupitia akaunti ya malengo kwa ajili ya ada za watoto wake lengo ambalo alifanikiwa kulitimiza.

"Nashukuru pamoja na kufanikiwa kulipa ada za watoto wangu kupitia akaunti ya malengo pia nimefanikiwa kupata zawadi ya gari litakalonisaidia kuwafikia zaidi wateja wangu huko mitaani. Nashukuru kwa kuwa zawadi hii itanirahisishia 'Kushinda mechi zangu", alisema Kweka.




Kiungo wa Manchester United, Kobbie Mainoo (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Crystal Palace, Chris Richards, kwenye nechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford jana. Crystal Palace ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Morrison aitupia Yanga kijembe

**Na Adam Fungamwango**

KUELEKEA mchezo wa keshokutwa kati ya Yanga na KenGold FC, utakaochezwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, winga mpya wa timu hiyo, Bernard Morrison ametupa kijembe kwa timu yake hiyo ya zamani, akisema siku hiyo timu yao itajulikana kwa jina la MC KenGold.

Morrison, ambaye anajulikana kwa vituko na vimbwanga, akiwa ndani na nje ya uwanja, ameandika kwenye mtandao wake wa kijamii, akisema inaonekana timu yake hiyo ya zamani inahofia timu zenye majina yanayoanzia na MC.

"Jumatano tutabadilisha tu jina letu kuwa ,MC KenGold' ili tupate matokeo mazuri. Kwa sababu inaonekana wanaogopa majina yanayoanza na MC," aliandika Morrison jana mchana, kitu ambacho kinaweza kufanya mchezo huo uwe gumzo na kuvutia mashabiki wengi.

Ikumbukwe kuwa Yanga ilitolewa kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kushindwa kutinga robo fainali baada ya kulazimishwa suluhu dhidi ya MC Alger ya Algeria, katika mchezo wa mwisho wa Kundi A, uliochezwa, Januari 8, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kabla ya hapo, ilifungwa mabao 2-0 na timu hiyo ikiwa ugenini, Desemba 7, mwaka jana, katika mfululizo wa michezo hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Iwapo atacheza, utakuwa ni mchezo wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu akiwa na timu hiyo, tangu alipojiunga nayo dirisha dogo la usajili.

"Mimi nimejiunga KenGold si kwa sababu ya pesa, au nimepata ofa nzuri, mimi nilikuwa majeruhi wa muda mrefu, niliumia wakati nipo FAR Rabat ya Morocco, sasa unapopona si vizuri kwenda kwenye timu kubwa ambazo zina presha na mahitaji makubwa, kwa hiyo nimekuja hapa kama mtu anayeanza upya maisha.

"Kitu muhimu ni kuisaidia KenGold kubaki kwenye ligi, siyo kwamba tumepata ofa nzuri sana," alisema mchezaji huyo raia wa Ghana.

Aliingia nchini akijiunga na Yanga 2020, alipocheza kwa nusu msimu kabla ya kuhamia Simba ambapo alicheza hadi 2022, aliporejea tena Yanga, akihudumu kwa msimu mmoja hadi 2023 na kutimkia FAR Rabat, kwa kuchukuliwa na aliyekuwa kocha wa timu hiyo, Nasreddine Nabi.

## Ramovic: Kikosi Yanga sasa ni moto mkali

INATOKA UK. 24

Sugar msimu huu, kwani katika mchezo wa mzuguko wa kwanza, ilishinda mabao 2-0, mechi iliyopigwa, Agosti 29, mwaka jana Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera, ambayo yalifungwa na Maxi Nzengeli na Mzize, ambaye aliifunga tena Kagera Sugar juzi.

Kwa sasa Yanga imefikisha pointi 42, kwa michezo 16 iliyocheza, ikishinda mechi 14, ilipoteza miwili, haijatoka sare, ikifunga mabao 36 na kuruhusu sita wavuni mwake.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Melis Medo, alisema bao la kwanza la kizembe waliloruhusu, ndilo lililowaondoa mchezoni.

"Goli la kwanza tuliruhusu kirahisi, baada ya hapo kila kitu kikaenda nje ya mipango, siwezi kusema sana, lakini nina uhakika kuwa penalti walizopata walizawadiwa, hazikuwa sahihi, hasa ile ya pili ambayo walifunga bao, lakini nawapongeza kwa ushindi," alisema Medo.

Yanga ilipata penalti mbili kwenye mchezo huo, moja ilikoswa na Stephane Aziz Ki, nyingine ikiwekwa wavuni na Pacome.

Kagera Sugar inasalia nafasi ya 15, ikiwa na pointi 11, ikicheza michezo 16, ikishinda miwili, sare tano na kupoteza michezo tisa.

## Simba hii hata 'Nyuki' inaua tu

INATOKA UK. 24

lilifanywa dakika ya 30, wakati Offen Chikola, alipoupata mpira uliopigwa kichwa vibaya na Abdulrazack Hamza.

Akiwa pembeni kidogo, takriban yadi 30, aliachia shuti kali lililopaa juu kidogo ya lango la Simba.

Ateba alifunga bao la pili kwa mkwaju wa penalti dakika ya 33, lililotokana na beki Pemba Kingu, kumuangusha Mpanzu ndani ya boksi.

Linakuwa ni bao la saba kwa Ateba kwenye msimamo wa Ligi Kuu msimu huu, akiwa ndiyo kwanza amesajiliwa mwanzoni mwa msimu akitokea USM Alger ya Algeria.

Anakuwa kwenye nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji, akiwa na mabao sawa na mwenzake wa Simba, Jean Ahoua na Clement Mzize wa Yanga, huku kinara wao akiwa ni Elvis Rupia, Mkenya anayeichezea Singida Black Stars mwenye mabao manane.

Kapombe aliifungia Simba bao la tatu, likiwa ni la pili kwake msimu huu, akiunganisha pasi murua kutoka kwa Ateba.

Kazi nzuri iliyofanywa na Mpanzu ambaye jana alihusika katika mabao yote matatu, alimpenyezea Ateba, aliyeonekana kuwa kwenye jitihada za kutaka kupiga shuti na kufunga kiasi cha mabeki wote wa Tabora United kumkaba yeye, lakini alichofanya ni kuuachia mfungaji aliyekuwa peke yake, akaukwamisha wavuni.

Timu zote zilifanya mabadiliko kadhaa yaliyoufanya mchezo kuchangamka zaidi, huku kipa Moussa Camara akifanya kazi ya ziada dakika tano za mwisho, kwa kuchumpa na kukoa mashuti ya hatari kutoka kwa Nelson Munganga na Rajab Masinga.

Ahoua pia alikaribia kufunga dakika za majeruhi kwa mpira wa mbali baada ya kipa kuonekana kusogea mbele ya lango.

Pamoja na kupoteza, Tabora United inabaki kwenye nafasi ya tano, ikiwa na pointi zake 25, kwa michezo 16 iliyocheza hadi sasa.

Michezo

Jumatatu Februari 3, 2025

Nipashe

## Ancelotti alia na rafu mbaya kwa Mbappe

UKURASA 21



# Simba hii hata 'Nyuki' inaua tu

## ●●● Ateba, Kapombe waionesha Tabora United kwamba wazichezee Yanga na Azam ila si Mnyama ambaye...

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 3-0 iliyoupata Simba jana dhidi ya Tabora United kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora, umedhihirisha kuwa ‚Nyuki' hao wa Tabora, si lolote kwa ‚Mnyama' huyo hatari anapokuwa mawindoni kusaka alama tatu katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

Kwa ushindi huo umeifanya Simba kurejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya Yanga juzi kukalia nafasi hiyo kwa muda kutokana na ushindi wao wa mabao 4-0 dhidi ya Kagera Sugar na kufikisha pointi 42, mchezo ukichezwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Katika mchezo huo wa Simba, yalikuwa ni mabao ya straika raia wa Cameroon, Leonel Ateba, aliyepachika mabao mawili na beki wa kulia, Shomari Kapombe, yaliyoifanya Simba kufikisha pointi 43, yakizima tambo za zaidi ya wiki moja za viongozi na mashabiki wa Tabora United.

Tabora United ilipata jeuri baada ya kuichapa Yanga mabao 3-1 na kisha kutoa kipigo cha 2-1 dhidi ya Azam FC kwenye mechi za mzunguko wa kwanza, matokeo yaliyoifanya kujiaminisha kwamba itaitandika pia Simba.

Kipigo hicho cha Tabora United kilifanana na kile cha mzunguko wa kwanza kilichotokea Agosti 17, mwaka jana, Uwanja wa KMC Complex, kwa mabao ya Che Fondoh, Malone, Velentino Mashaka na Awesu Awesu.

Kwa maana hiyo, Simba imezoa pointi zote sita na mabao sita msimu huu kutoka kwa ‚Warina Asali' hao wa Tabora.

Pia Simba imerudia ilichokifanya msimu uliopita kwenye uwanja huo huo, Februari 6, mwaka jana, ilipoichakaza Tabora United mabao 4-0, yaliyowekwa wavuni na Pa Omar Jobe, Sadio Kanoute, Fredy Koublan na Che Malone.

Purukushani za Ateba kwenye lango la Tabora United zilianza dakika ya tatu tu ya mchezo, pale alipofanikiwa kuruka juu na kupiga kichwa mpira mrefu uliopigwa na Fabrice Ngoma, ukampita kipa, Jean Noel Amonone, lakini wakati ukielekea wavuni ulitokolewa na beki Nelson Munganga.

Simba ilifanya shambulio lingine dakika nne baadaye, wakati Elie Mpanzu alipoambaa na mpira kwenye winga wa kushoto, akapiga krosi iliyokuwa ikisubiriwa kwa hamu na wachezaji wenzake, lakini kipa Amonone, raia wa Gabon, aliyesajiliwa kipindi cha usajili wa dirisha dogo kutoka Arta Solar ya Djibouti, akawahi kuudaka.

Kichwa cha Kibu Denis pia kilidakwa na kipa huyo dakika ya nane, naye akiwekewa pasi ndefu ya juu na Ngoma.

Simba iliandika bao la kwanza dakika ya 12, mfungaji akiwa ni Ateba, kwa shuti kali la chinichini lililoonekana kama linakwenda nje, lakini mpira ukajaa ndani ya wavu.

Kabla ya kufunga alikuwa amepokea pasi kutoka kwa Mpanzu, akageuka na kuwahadaa mabeki wa Tabora United kabla ya kupachika mpira huo, kipa akiruka bila mafanikio.

Shambulio la kwanza la hatari kwa Tabora United kwa Simba

INAENDELEA UK. 23



Mshambuliaji wa Simba, Lionel Ateba, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la kwanza wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Tabora United, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, mjini Tabora jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Ramovic: Kikosi Yanga sasa ni moto mkali

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Kagera Sugar, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amekisifu kikosi chake, akisema sasa kimekuwa moto wa kuotea mbali, akikiri kuwa kimebadilika na kucheza lile soka ambalo amekuwa akilihitaji tangu alipofika nchini.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo uliopigwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi, kocha huyo alisema kama wataendelea kucheza kwenye kiwango hicho, basi ana uhakika wa kutimiza malengo yote yaliyosalia, kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara na Kombe la FA.

"Nichukue nafasi hii kwa kuwapongeza wachezaji wangu, wamecheza vizuri, tulianza mechi vema, tukaitawala, tungeweza kufunga mabao matatu kabla ya bao la kwanza, wapinzani wetu walibaki nyuma ya mpira na kujaribu kutushambulia kwa kushtukiza na mipira ya faulo, lakini tulicheza kwa nidhamu kubwa.

"Niseme tu kuwa kwa sasa tuko kwenye njia sahihi, naona wachezaji wangu sasa wameanza kucheza soka ninalotaka na kwa kasi ninayoihitaji, wamebadilika, najivunia hilo, na ikiendelea hivi basi malengo yote yaliyobaki tuliyojiwekea yatatimia," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

Ulikuwa ni ushindi wa sita mfululizo kwa kocha huyo kwenye michezo ya Ligi Kuu, tangu alipotua nchini na kukianza kukinoa, akichukua nafasi ya Miguel Gamondi, ambaye aliondolewa pale ilipopoteza kwa kufungwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United, Novemba 7, mwaka jana.

Kocha huyo aliiongoza Yanga kushinda mabao 2-0 dhidi ya Namungo FC, Uwanja wa Ruangwa, Lindi, ikazichapa Mashujaa FC 3-2, Prisons 4-0, Fouintain Gate 5-0, na Kagera Sugar 4-0, mechi zote zikipigwa Uwanja wa KMC Complex, uliopo Mwenge, Dar es Salaam, na Dodoma Jiji ambao walilala 4-0, mechi iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Katika michezo hiyo sita, Yanga imefunga jumla ya mabao 22, ikiruhusu mawili tu.

Yalikuwa ni mabao ya Clement Mzize, Mudathir Yahaya, Pacome Zouzoua na Kenndy Musonda.

Ushindi huo umeifanya Yanga kuzoa pointi zote sita kutoka kwa Kagera

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA

9 770856 541002 >